Kutoka Msalabani hadi Utukufuni

Mafunzo juu ya Utakaso

“Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.” Waebrania 10:14

Paulo Galligan
Huduma ya Ufuvio Australia

YALIYOMO

UTANGULIZI: **Kutoka Msalabani hadi Utukufuni**

SURA YA KWANZA: **Kuhesabiwa Haki**

SURA YA PILI: **Utakaso**

SURA YA TATU: **Kutakaswa kwa Damu**

SURA YA NNE: **Kutakaswa kwa Neno**

SURA YA TANO: **Kutakaswa kwa Roho**

SURA YA SITA: **Kuingia katika Utukufu**

UTANGULIZI

NENO WA MSALABA

"Kwa sababu Neno la Msalaba kwao wanaopotea ni upuzi, bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu." **1 Kor 1:18.**

Neno la Msalaba ni la msingi na kuu katika kuendeleza ujumbe wa Injili na Neno la Mungu. Kupitia kwa kifo cha Yesu Msalabani na kufufuka kwake kutoka kwa wafu, tunaokolewa kutoka kwa dhambi na kwa njia ya ubatizo tuna unganishwa na Kristo, kwanza katika kufa na kuzikwa Kwake na pili katika Kufufuka Kwake katika wafu. Katika ubatizo wa maji, tunaufahamu msalaba; kabla ya ubatizo tunatakiwa kutubu dhambi na tumpokee Yesu; tunatakiwa '***tuzaliwe mara ya pili'*** (**Yohana.3:3**), lakini Maandiko Matakatifu yanafundisha kuwa **njia ya kuwa seshemu ya kanisani ni kwa njia ya ubatizo** (**Matendo 2:41**), kwa sababu katika ubatizo tunakufa na Kristo, tunazikwa na Kristo na tunafufuka na Yesu Kristo.

Warumi 6:4-5 ***"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake.***

UJUMBE WA MSALABA UNABAKI KUWA UJUMBE MKUU

Katika kuelezea Neno la Mungu na ufunuo wa makusudi Yake ya kinabii, ujumbe wa Msalaba unabaki kuwa mkuu. Katika Sikukuu tatu za Israeli, Pasaka, Pentekoste [sikukuu ya majuma] na Sikukuu ya Vibanda, makuhani walitakiwa kutoa sadaka ya kuteketeza. Maelezo juu ya Sadaka ya kuteketezwa au dhabihu yamo katika **Kutoka 29:38-46.** Sadaka ya kuteketezwa ilikuwa ya Mwana kondoo wa mwaka mmoja aliyechinjwa asubuhi na Mwana kondoo wa pili alichinjwa jioni; pamoja na Mwana – kondoo kulikuwa na sadaka ya unga mzuri uliochanganyika na mafuta yenye kuponda na sadaka ya kinywaji [divai **Mwana-kondoo anatuelekeza kwa Mwana-kondoo wa Mungu achukuaye dhambi za dunia**, (**Yohana 1:29)**. Sadaka ya kuteketeza ndiyo iliyokuwa kuu katika kila sehemu ya hizo Siku kuu. Hili linatufundisha kuwa msalaba unabaki kuwa kuu hata tunapoendelea na safari ya kuzitimiza zile Siku kuu zingine.

YESU ALITUPATIA MEZA MSALABA UKIWA NDIO MKUU

Bwana Yesu usiku ule aliotolewa, alitwaa mkate na divai, akasema, "***Huu ndio Mwili Wangu na damu Yangu***" ambavyo tunastahili kushiriki, tukimukumbuka.**Matt.26:26-28**).

Ujumbe wa Msalaba umejumuishwa ndani ya Meza ya Bwana. Meza ya Bwana ni lazima iwe kuu, katika mkusanyiko wowote wa waaminio. Ni mojawapo ya "***matendo ya kwanza***" ya msingi (**Ufu.2:5)** ya Kanisa la Agano Jipya. **Matendo 2:42** ***"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega Mkate, na katika kusali."*** Katika Kanisa la kwanza, **"kuumega mkate"**, [ushirika katika Mwili na Damu ya Bwana wetu Yesu Kristo] lilikuwa tendo la kila siku, (**1 Kor.10:16, Matendo 2:46)**.

Katika **Yohana 12:32**, Yesu akasema ***"Nami nikinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu."*** Katika **aya ya 33** Yohana anatwambia kuwa Yesu alikuwa akizungumzia namna ya kifo Chake, naam, kifo Chake Msalabani.

MSALABA UNAHUBIRIWA KUPITIA KATIKA MEZA YA BWANA

Ujumbe wa msalaba ni ujumbe wa wokovu, lakini ni watu wachache wanaotambua kuwa ujumbe wa msalaba unaonekana wazi katika Meza ya Bwana. Kila wakati tunapoumega mkate na kushiriki kikombe, tunaitangaza '***mauti ya Bwana hata ajapo'*** (**1 Kor.11:26**).

MEZA YA BWANA NI UINJILISTI!
Meza ya Bwana haitakiwi kuwa radhi ya kidini kwa wale wachache waliojaaliwa, bali **sherehe ya Meza ya Bwana inatakiwa kutumiwa kama sehemu ya makali ya injili; kuwahubiri waliopotea ujumbe wa msalaba.** Yesu Kristo anapaswa kuinuliwa katika ***Ushirika wa Meza***, naye atawavuta waliopotea, jinsi alivyoahidi.

KUHESABIWA HAKI MSALABANI
Pale msalabani tunaokolewa. Kupitia kwa kufa na kufufuka kwa Bwana wetu Yesu Kristo, tunahesabiwa haki. Maandiko Matakatifu yanasema **[Warumi 4:25]** kuwa ***'Alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili mpate kuhesabiwa haki'***. Kwa hivyo kupitia kwa imani ndani ya Yesu Kristo, kifo Chake cha upatanisho na kufufuka kwake kwaushindi, tuna amani na Mungu na tunaokolewa.

MEZA YA BWANA INAWAVUTA WALIOPOTEA
Tunatambua na kufahamu kutokana na historia kuwa Meza ya Ushirika ni mahali pa ushirika wa karibu na Bwana wetu Yesu Kristo na waaminio waliokusanyika mahali patakatifu pa Mungu. ***Meza ya Ushirika*** ilifanyika pale kwenye ***Meza ya mikate ya wonyesho*** katika Mahali Patakatifu pa Hema ya Musa. Pia tunashuhudia kwamba katika kuinuliwa kwake Yesu, kumukumbuka katika ushirik wa mkate na divai, ina nguvu za kubadilisha mazingira ya kiroho ya mahali na kushika akili za watu waliopo, wawe ni wa Kikristo, Kiislamu, Kibuda au watazamaji tu ambao hawaja amua.

Meza ya Bwana yaweza kusherehekewa palipo na wawili ama watatu ambao wamekusanyika katika Jina Lake na kumukumbuka katika mkate na kinywaji. Mkate na divai wakati mwingine yawezakuwa biskuti na maji ya machungwa, au wali wakati mkate haupatikani, au kahawa na viazi.

Kwa vyo vyote vile na Popote pale ambapo waaminio wanakusanyika kumukumbuka Yesu, Mwana – Kondoo wa Mungu aliyezichukuwa dhambi za dunia,
alipokufa kama Azazeli msalabani,
na kuhubiri ukombozi wa uweza wa damu Yake,
mapepo wanatoroka
mazingira ya kiroho yanabadilika,
nia za watu zinavutiwa na Yesu,
na Roho Mtakatifu anashuhudia.

YESU ANATAMBULIKA KATIKA KUUMEGA MKATE
Hili ndilio timizo la **Yohana 12:32**. Kumuinua Yesu juu! Kukumbuka na kuvutiwa kwa namna ya kifo Chake, na sababu ya kifo Chake. Hata wanafunzi waliokutana na Yesu wakienda kijiji kimoja kiitwacho Emau baada ya kufufuka kwake kutoka katika wafu walimtambua katika kuumega mkate, kwa hivyo hata sasa watu wanavutwa kwake Yesu kwa sababu ya ufunuo waa Yesu katika Meza ya Ushirika.

SAFARI INAANZIA MSALABANI
Wanaisraeli walikombolewa [waliokolewa] kutokana na maangamizi ya Misri, kwa damu ya Mwana-kondoo waPasaka kwenye miimo na visingiti vya milango yao, na nyama ya Mwana-kondoo walioila ya kuwatia nguvu kwa ajili ya safari yao kutoka Misri. **Yesu aliitimiza Pasaka wakati damu Yake ilipomwagika msalabani.** Safari yetu ndani ya Mungu huanzia Msalabani, kama jinsi safari ya Wanaisraeli ilipoanza na Pasaka. Msalaba ndio ***mwanzo wa safari yetu***! Ujumbe wa Msalaba unabaki kuwa mkuu katika safari yetu, lakini tunaelekea wapi?

KUTUKUZWA NDILO LENGO

Biblia inasema, ***'na wale aliowachagua tangu asili, hao akawaita, na wale aliowaita, hao akawahesabia haki; na wale aliowahesabia haki, hao akawatukuza'*** (**Warumi 8:30**). Kuhesabiwa haki hakika huja kwetu kwa njia ya kufufuka kwa Yesu katika wafu. Alikufa na akamwaga damu Yake ili akabiliane na dhambi zetu, alifufuka ili atupatie uzima. Tumehesabiwa haki pale msalabani. Lakini Biblia pia inatwambia tunatukuzwa. Tunastahili kuelewa jinsi ya kutukuzwa. Hili ndilo lengo la Mungu kwetu. Safari ni kutoka Msalabani hai Utukufuni. Lakini tutfikaje hapo?

YESU ANARUDIA KANISA TUKUFU

Yesu analirudia Kanisa tukufu, kwa hivyo kutukuzwa ni lengo letu hapa duniani. Lengo la Mungu kwa Kanisa Lake limefunuliwa kwetu katika **Efe.5:27**. Anajiandalia "***Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa."***

NI NINI TUMAINI LA MWITO WETU?

Tumeitwa kusafiri kuelekea UTUKUFUNI.

Paulo anatuombea katika **Waefeso 1:18,** kuwa tujue ***"tumaini la mwito wake"***, ambalo ni ***"Kristo ndani yetu ni tumaini la utukufu"*** na kisha anaomba kuwa tujue utajiri wa utukufu wa Mungu na urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo. Sehemu ya safari ya utakaso ni macho ya mioyo yetu kutiwa nuru, tujue tumaini la utukufu ambao Paulo anazungumzia. **Kol.1:27** ***"Ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utkufu."***

Hili tumaini tena linazungumziwa katika **Waebrania 6:19** ***"Tumaini hili tulilo nalo ni kama nanga ya Roho, yenye salama, yenye nguvu, yaingiayo hata mle mlimo ndani ya pazia."*** Nanga ya nafsi zetu imo ndani ya utukufu.

1 Yohana 3:3 pia yazungumzia jambo hili, ***"kila mwenye matumaini haya katika yeye hujitakasa, kama yeye alivyo mtakatifu."*** Tumaini ni kuwa atakaporudi, tutafanana Naye. Tuna tumaini hili la nguvu kuwa Yesu anarudi tena. Kwa sababu ***tuna hilo tumaini, tunajitakasa.***

TUNATUMAINIA UTUKUFU WA MUNGU KUJA

Mwito Wake ni kwamba Anataka tuje utukufuni. Tumaini hili halimo katika kitu ambacho tayari kinaonekana; hili ni tumaini lililo katika kitu kisicho kuwa na mwisho, (**2Kor.4:18**).

Tito 2:13 analiita hili **t**umaini 'tumaini lenye baraka', ***"tukilitazamia tumaini lenye Baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu."***

URITHI WA UTUKUFU NA NGUVU KUU

Paulo pia anatuombea katika **Efe.1:18** ya kwamba tutajua ***"utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu."*** Paulo anatwambia kuwa ***Mungu ana uruthi ndani yetu.*** Unapoachana na maisha ya kale na ufanyike muumini aliyezaliwa mara ya pili, Mungu anakuwa amepokea urithi Wake. Huu ni urithi wa utukufu.

Paulo tena anataka tujue ***"na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio"*** (**a.19**). Huu pia ni ***urithi wa nguvu***.

NI SAFARI YA UTAKASO

Katika funzo hili tunafumbua funzo la utakaso. Ni kupitia katika utakaso wa Baba, kupitia utakaso wa damu ya Yesu, utakaso wa Neno na pia kupitia katika utakaso wa Roho Mtakatifu, ili tusafiri kutoka Msalabani hadi Utukufuni.

Waebrania 10:14 ***"Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa."*** Tena msalaba ndio mkuu katika safari yetu kuelekea utukufuni bali tunarithi tu '***timilifu'*** tunaposafiri katika ukweli wa utakaso. Tunapoishi katika mafunzo yaliyo ya kweli ya Neno la Mungu, tunapoendelea kushuhudia nguvu za utakaso katika Damu, Neno na Roho Mtakatifu, tutaendelea mbele tuufikilie utimilifu na tuanze kung'aa kama "MWANA". Ikiwa tuna maono ya utukufu wa Mungu kufunuliwa, basi kwa ujasiri tutaendelea na safari katika utakaso ili tufikie utimilifu wa ahadi za Mungu ambazo ni tukufu (**2Pet.1:4**).

SURA YA 1

KUHESABIWA HAKI

KUHESABIWA HAKI KATIKA YESU KRISTO

Mtumishi wangu mwenye haki atawafanya wengi kuwa wenye haki.
Isaiah 53:10-12 ***"Lakini BWANA aliridhika kumchubua; amemhuzunisha; utakapofanya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi, ataona uzao wake, ataishi siku nyingi, na mapenzi ya BWANA yatafanikiwa mkononi mwake; ataona mazao ya taabu[utungu] ya nafsi yake, na kuridhika. Kwa maarifa yake mtumishi wangu, Mwenye haki atawafanya wengi kuwa wenye haki; naye atayachukua maovu yao. Kwa hiyo nitamgawia sehemu pamoja na wakuu, naye atagawanya nyara pamoja nao walio hodari; kwa sababu alimwaga nafsi yake hata kufa, akahukumiwa pamoja na hao wakosao. Walakini alichukua dhambi za watu wengi, na kuwaombea wakosaji."***

Maandiko Matakatifu yanasema kuwa Yesu '***atawafanya wengi kuwa wenye haki'***. Atafanya hivyo kwa njia gani? ***"Atayachukua maovu yao,"*** kwa kufanya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi.
Mafunzo ya utakaso katika lugha ya kawaida ni: kuhesabiwa haki na Mungu; dhambi zetu zote kuondolewa.

MTU AWEZAJE KUHESABIWA HAKI MBELE YA MUNGU?
Kupitia kwa imani ***katika kufa na kufufuka kwake Bwana wetu Yesu Kristo;*** kwa kuamini ujumbe wa Injili kwamba Kristo aliteseka, akafa na akafufuka siku ya tatu.

Vivungu hivi kutoka kwa chuo cha **Isaya** yatuonyesha jinsi ambavyo Yesu alipata kutuleta mahali pa kuhesabiwa haki.
a10 Kwa kufanya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi: BWANA aliridhika kumchubua, Akamhuzunisha. Matokeo ya hayo ni kwamba ataona uzao wake, ataishi siku nyingi.
a11 Wakati Yesu alipoifanaya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi, **haki ya Mungu aliridhisha**, na aliweza kutusamehe. Yesu alichukua maovu yetu. Msingi wa ujumbe wa kuhesabiwa haki ni neno la Msalaba.

Paulo anasema katika **1Kor.2:2** ***"Maana naliazimu nisjue neno lo lote kwenu, ila Yesu Kristo, naye amesulubiwa."***

Isa.53:12 Yesu alimimina nafsi yake hata kufa. Akahesabiwa pamoja na hao wakosao.
2Kor.5:21 ***"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye."***
Alifanyika dhambi kwa ajili yetu ili sisi tupate na kujitambulisha na haki Yake.

YESU MPATANISHI
Jesus made intercession for the transgressors. An intercessor is one who stands in the gap. **1Tim.2:5-6** ***"Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Yesu Kristo, ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote atakaoshuhudiwa kwa majira yake."*** Yesu alisimama katika pengo kwa ajili yetu.

Filip.2:8 ***"Tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba."*** Yesu alitufia.

KUHESABIWA HAKI KATIKA AGANO LA KALE

Habakuki alitangulia kuona maisha ya imani ambayo yanatokana na kuhesabiwa haki.
Hab.2:4 ***"Tazama roho yake hujivuna, haina unyofu ndani yake lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake."*** ***W***enye haki, wataishi.

Wasio haki au waovu wataangamia kwa sababu ya kutokuamini.

Kuhesabiwa haki huanzia pale Yesu alipojitoa Msalabani kama dhabihu; hatua yetu ya pili ni ***kuamini***; kwa hiyo imani ndani yake tumehesabiwa haki na kwa hiyo tutaishi.

> **Haki,** *tsaddiq,* (tsahd-deek) Strong's #6662: Kweli, haki, safi; mtu mwenye tabia ya usawa, mnyofu na wa haki katika mambo yake. Laonekana zaidi ya mara 200, *tsaddiq* linatokana na kitendo *tsadaq,* "kuwa mwenye haki, msafi, kweli." *Tsadaq* pamoja na hayo mengine huwakilisha haki na unyofu katika maisha ya mtu. Kuwa mtu wa haki humletea mtu nuru na furaha. *Tsaddiq* laonekana mara 66 katika kitabu cha Mithali pekee yake.

Mithali.4:18 ***"Bali njia ya mwenye haki ni kama nuru ing'aayo, ikizidi kung'aa hata mchana mkamilifu."*** Mchana mkamilifu ni wakati Yesu atakapojitokeza kutupeleka kikamilifu katika utukufu wake. Tuko njiani, safarini, kutoka msalabani hadi utukufuni; na inaanza na kuhesabiwa haki.
Mithali.24:16 ***"Kwa maana mwenye haki huanguka mara saba akaondoka tena; bali wasio haki wanakwazwa na mabaya."*** Japo mwenye haki ataanguka, Bwana atamuinua tena, maana amehesabiwa haki. Ameweka tumaini lake katika yeye aliyesulubiwa.

NUHU ALIKUWA MTU MWENYE HAKI: ALITEMBEA NA MUNGU

Mwa.6:9 "Hivi ndivyo vizazi vya Nuhu. Nuhu alikuwa mtu wa haki, mkamilifu katika vizazi vyake; Nuhu alikwenda pamoja na Mungu." Nuhu alikuwa muhubiri wa haki katika kizazi chake. Mungu anataka Kanisa lake la nyakati za mwisho liwe la wahubiri wa haki katika kizazi chetu, tukiwaambia watu kuhusu Yesu Kristo, na kujiandaa kwa kurudi Kwake tena.

'Kutembea na Mungu' ni nini?

Hii ni safari ya utakaso tukiwa safarini kutoka msalabani [kuhesabiwa haki] hadi utukufuni. Nuhu ni mtu aliyekwenda na Mungu; alikuwa ametakaswa na Mungu.alijitenga kwa ajili ya Mungu. **Kuenda kwetu na Mungu = *Utakaso.*** Katika safari yetu na Mungu tunatakaswa. Wakati wanaisraeli walipoufikia Mlima Mtakatifu wakiwa safarini kuelekea Nchi ya Ahadi, kazi ya utakaso ilianza maishani mwao maana Mungu mwenyewe alijufunua kwao kama ***"BWANA awatakasaye"*** **Walawi.20:8**. Hii kazi hakika ilianza wakati wana waisraeli walipoiweka damu ya Mwana-kondoo katika nyumba zao – walitengwa kutokana na hukumu kupitia kwa hiyo damu.

IBRAHIMU, MTU MWENYE HAKI

Mwa.15:1-6 yazungumzia juu ya Agano la Mungu na Abramu. Abramu aliamini yale Mungu alimwambia, **ay.6** ***"Akamwamini BWANA, naye akamuhesabia jambo hili kuwa haki."***
Ibrahimu hakuhesabiwa haki kwa matendo yake, bali kwa imani yake kwa Mungu.
Rum.4:2-3 ***"Kwa maana ikiwa Ibrahimu alihesabiwa haki kwa ajili ya matendo yake, analo la kujisifia; lakini si mbele za Mungu. Maana Maandiko yasemaje? Ibrahimu alimwamini Mungu akihesabiwa kwake kuwa haki.'"*** Kuhesabiwa huku kwa imani kulitangulia sheria. Baba yetu Ibrahimu, kulingana na **Mwa.15:6** aliamini Mungu na akahesabiwa haki. Katika **Rum.4** Paulo anatuonyesha urithi wa imani kama msingi wa haki, badala ya sheria, ni urithi tulio nao kutoka kwa Ibrahimu.

KUHESABIWA HAKI KATIKA AGANO JIPYA

KUMUAMINI YEYE

Rum.4:23-25 Paulo anazungumzia haki ambayo Ibrahimu alihesabiwa, ***"Walakini haikuandikwa kwa ajili yake tu kwamba ilihesabiwa kwake; bali na kwa ajili yetu sisi mtakaohesabiwa vivyo hivyo, sisi tunaomwamini yeye aliyemfufua Yesu Bwana wetu katika wafu; ambaye alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili mpate kuhesabiwa haki."*** Wote waamino wanaweza kuhesabiwa haki jinsi Ibahimu alivyo hesabiwa haki. Tunaamini nini? ***"Tunamwamini yeye aliyemfufua Yesu Bwana wetu katika wafu."***

KUHESABIWA HAKI ITOKAYO KATIKA IMANI

Rom.5:1 ***"Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na imani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo."***
Tunahesabiwa haki itokayo katika imani**,** hii inatupatia amani na Mungu.

KUHESABIWA HAKI HULETA UPATANISHO

a2-5 Inazungumzia juu ya 'mwenendo' ambao tunastahili kuwa nao katika safari ya utakaso ambao tutaangalia kwa makini katika sura nyingine.
a6-8 Tulipokuwa bado wenye dhambi, ***Mungu alionyesha pendo lake*** kwetu kwa kumruhusu Yesu kutufia.
a9-11 Sisi tuliostahili kufa kwa sababu ya makosa yetu tumehesabiwa haki kwa njia ya damu yake. Tulikuwa maadui wake Mungu lakini tumepatanishwa na Mungu kupitia kwa kifo chake Yesu. Sisi sio maadui Wake tena; tumefanyika marafiki Wake.

<u>Kuhesabiwa haki huleta upatanisho</u>.

UZIMA BADALA YA MAUTI

v12-17 Kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti. Lakini Mungu ashukuriwe, Yesu alikuja kutuokoa kutoka kwa dhambi na madhara yake. Badala ya mauti tuna uzima. ***"Wala kadiri ya Yule mtu mmoja aliyefanywa dhambi si kadiri ya kile kipawa; kwa maana hukumu ilikuja kwa njia ya mtu mmoja ikaleta adhabu; bali karama ya neema ilikuja kwa ajili ya makosa mengi, ikaleta kuhesabiwa haki."*** **[v16]**.

<u>Kuhesabiwa haki kulileta mabadiliko; uzima kwa mauti</u>.

v18 ***"Basi tena, kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu, kadhalika kwa tendo moja la haki watu wote walihesabiwa haki yenye uzima."***

SIO KWA MATENDO

Gal.2:16 ya tilia mkazo funzo la kuhesabiwa haki, ***"Hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu; sisi tulimwamini Kristo Yesu ili tuhesabiwe haki kwa imani ya Kristo, wala si kwa matendo ya sheria; maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki."***

<u>Tumehesabiwa haki itokayo katika imani ndani ya Yesu Kristo</u>,
na sio kwa matendo ya sheria!

Rum.3:20 ***"Kwa sababu hakuna mwenye mwili atakaye hesabiwa haki mbele zake kwa matendo ya sheria; kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria."***

KIPAWA CHA NEEMA YAKE

Rum.3:23 Yatuambia kuwa ***"wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu,"*** bali ***"wamehesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu,"*** **v.24**.

Sisi **<u>kuhesabiwa haki ni kipawa cha bure ambacho tumepewa kwa Neema Yake!</u>**

MUNGU NI MWENYE HAKI NA AMEFANYIKA MWENYE KUMHESABU HAKI
Aya za 25 & 26 zaendelea kusema kuwa Mungu alimweka Yesu Kristo***"awe upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake, ili aonyeshe haki yake, kwa sababu ya kuziachilia katika ustahimili wa Mungu dhambi zote zilizotangulia; apate kuonyesha haki yake wakati huu, ili awe mwenye haki na mwenye kumhesabu haki yeye amwaminiye Yesu."***

KUMALIZIA KWA MAFUNZO YA PAULO
Rum.3:28 ***"Basi twaona kuwa mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria."***

KUENENDA KATIKA IMANI IONGEZEKAYO
Rum.1:16-17 ***"kwa maana siionei haya injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia. Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hadi imani; kama ilivyoandikwa, 'mwenye haki ataishi kwa imani.'"***

HUKUMU - KWA YULE ASIYEAMINI
Yohana 3:36 ***"Aaminiye yuna uzima wa milele; asiyeamini Mwana hana uzima wa milele, bali gadhabu ya Mungu inamkalia."***
Kinyume cha kuhesabiwa haki ni *hukumu*. Ukiwa unatembea katika hukumu, gadhabu ya Mungu iko juu yako.

HUKUMU - JUU YA YULE ANAYESITA-SITA
Heb.10:37-38 ***"Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana, Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia. Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; naye akisita-sita, roho yangu haina haja."***
Njia ya kumpendeza Mungu ni kuamini katika kufa na kufufuka kwake Yesu Kristo, Mtumishi anayeteseka wa **Isaya 53**.

SAFARI INAANZIA MSALABANI:

Tunaokolewa, tunahesabiwa haki msalabani. Safari inaanzia msalabani. Wakati Paulo mtume alipokuwa Korintho mara ya kwanza, alihubiri msalaba, ***"Kristo Aliyesulubiwa."*** Watu wengi waliokolewa kwa sababu Roho Mtakatifu aliuthibitisha ujumbe wa msalaba na ishara zikifuata. Lakini Paulo hakuwaacha Wakorintho msalabani. Anasema ***"walakini iko hekima tusemayo kati ya wakamilifu"*** (**1Kor.2:6**); kuna ziada!

Kuna mahali pa kuenda, kukua katika utimilifu.

NENO LA MSALABA:
Wakorintho waliokolewa kupitia Neno la msalaba; ujumbe wa kuhesabiwa haki ulihubiriwa. Lakini Paulo aliendelea kuwafundisha mambo mengi kutoka kwa Neno la Mungu ili waendelee kukua. Katika **2Kor.3:18**, Paulo anawausia wakorintho kuwa lengo ni ***"kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, toka utukufu hadi!"***

Paulo anawaambia Warumi kuwa tumeitwa na Mungu katika Makusudi Yake. ***"Na wale aliowachagua tangu asili, hao aliwahesabia haki pia, na wale aliowahesabia haki, hao akawatukuza."*** Kusudi la Mungu ni kuwatukuza wale aliowaita. Mwisho wa safari ni kutukuzwa!

SURA YA 2

UTAKASO

Rum. 8:29-30 ***"Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili Yeye awe Mzaliwa wa Kwanza miongoni mwa ndugu wengi. Na wale aliowachagua tangu asili, hao akawaita, na wale aliowaita, hao akawahesabia haki; na wale aliowahesabia haki, hao akawatukuza.'***

LENGO LA MUNGU KWETU

Lengo la Mungu kwetu ni tufanane na Yesu, tukifanyika Mtu Mpya ambaye ameumbwa katika mfano na sura ya Mungu. Lengo la Mungu kwa Kanisa lake kwa jumla ni lifikilie ukamilifu ***"hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo,"*****(Efe.4:13)**. Watu wengi hudhani kuwa kuihubiri injili ndilo lengo lengo la Mungu. Kuihubiri injili kwa mataifa yote ni amri yake Bwana kwetu sisi katika **Marko 16:15-16**. Bali tume kuu katika Mathayo inatuamurisha kuwafanya wanafunzi, ***"na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi."*** **Matt.28:20**.

<u>Kusudi la Mungu ni katika njia mbili</u>:
*** kuihubiri injili kwa kila nafsi,** kama ushuhuda kwa mataifa yote (**Matt.24:14**);
*** kulileta Kanisa katika utimilifu** (**Ebr.6:1, Efe.4:11-16**).

MUNGU ALITUJUA TANGU ASILI
(a) Mungu alitujua tangu asili na kwa msingi huo, **<u>alituwekea hatima</u>** ilitufananishwe na mfano wa Mwana wake. Huku kujua kwa Mungu uko juu ya msingi Wake kuwa wakati Fulani katika maisha yetu, tutamuitikia Yesu Kristo. Kwa sababu alijua haya tangu asili, alikusudia tufananishwe na Mwanawe Yesu.

Huku kutuhatimisha uko juu ya msingi wa Mungu wa kutujua tangu asili kuwa tutachagua kufananishwa na Mwana wake. Tume hatimishwa ili tufananishwe na mfano wa Mwanawe ili awe Mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.

MUNGU AMETUITA
(b) Katika msingi wa kutujua tangu asili kwa kile tutafanya baada ya kuipokea injili, **Mungu alituita.** Mungu alitoa mwito; bali alituwacha tusikie atuitapo.

MUNGU AMETUHESABIA HAKI
(c) Wale aliowaita, **Mungu aliwahesabia haki**
Yesu alitolewa kwa ajili ya makosa yetu bali Mungu alituhesabia haki kwa kumfufua Mwana Wake kutoka kwa wafu.
Warumi 4:24-25 ***"Sisi tunaomwamini yeye aliyemfufua Yesu Bwana wetu katika wafu; ambaye alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili mpate kuhesabiwa haki."***
Rum. 5:1 ***"Basi tukiisha hesabiwa haki, itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo."***

<u>Tunapokea kuhesabiwa haki kwa imani.</u>

MUNGU PIA AMETUTUKUZA
(d) Na hao aliowahesabia haki, hao pia **aliwatukuza**.
<u>Hii ni kazi kamilifu.</u> Lengo la Mungu ni Bibi-arusi ambaye ni Kanisa tukufu. Maandiko Matakatifu yako wazi katika sehemu nyingi yakwamba tukaze mwendo tuufikilie utimilifu. Vivyo hivyo, maandiko pia ni wazi kuwa Mungu ametoa njia ambapo tunaweza kuufikia huo

ukamilifu. Jinsi tunavyohesabiwa haki kwa njia ya imani – kuwa ni kazi kamilifu pale Kalvari – vivyo hivyo ndivyo tunafikia kutukuzwa kwa njia ya imani.

TUTAFANANISHWA NA JINA LA JAMII
Tunapompokea Yesu kama Mwokozi [kuhesabiwa haki] na kama Bwana [kutukuzwa] tunazaliwa upya katika jamii ya Mungu na kwa hivyo tutakua tukufanana na Baba yetu, hivyo, ***"Tunafananishwa na mfano wa Mwana wake."***
Yoh. 1:12 "***Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio Jina Lake."***

RASLIMALI YOTE YA MUNGU INAPATIKANA
Kutimiza hili kusudi Lake la ajabu la kulitukuza Kanisa, Mungu amezifanya raslimali zake zote kupatikana kwa ajili yetu.
Maandiko Matakatifu yanasema katika **Warumi 8:31-38:**
a:31 kuwa ***Mungu yupo upande wetu***
a:32 kuwa ***atatukirimia mambo yote***
a:33 kuwa ***hakuna atakaye tushitaki***
a:34 kuwa ***tunaye Kuhani Mkuu*** rohoni
a:35-38 kuwa ***hakuna kitakachotutenganisha*** na upendo wa Kristo.
[Tunapoendelea kuujua ukweli wa Mungu zaidi na zaidi, mambo ambayo wakati mwingine tunayaruhusu kuleta mgawanyiko yataondoka.]

Tunaona kuwa kuhesabiwa haki na kutukuzwa ni kwa njia ya imani, lakini tutawezaje kutoka pale msalabani tulikohesabiwa haki hado utukufuni katika chumba cha Kiti cha Enzi cha Mungu?

SAFARI YA UTAKASO

Mwito wa Mungu ni kwa kila aaminiye na kwa Kanisa kuufikia ukamilifu au utimilifu. **Hii safari inaitwa safari ya utakaso.**

> *Maana ya 'utakaso' ni 'sadaka'. Kutengwa, kufanya takatifu.*
> *Katika kilatin neno 'sanctus' ndilo neno: 'takatifu'.*
> *Kwa hivyo tunapotakaswa, tunafanywa watakatifu. Tunatengwa kutokana na kila kisicho safi na kutengwa kwa ajili ya Mungu ambaye ni Mtakatifu.*

Tunatakaswa [tengwa] ili tukue kutoka kuwa wakristo wachanga hadi wakristo waliokomaa, zaidi na zaidi kama Yesu.
Tunatakiwa tutengwe kwa ajili:

* ya ***kutukuzwa***
* ya ***kuupokea utukufu wa Mungu***
* ya ***kujitolea kwa Bwana kikamilifu***
* ya ***kufananishwa na mfano wa Mwana Wake***

JE UTAKASO UNAFANYIKA JINSI GANI KATIKA MAISHA YETU?

Ni Mungu Baba ndiye atutakasaye (**Juda1**). Ni Yeye aliyesema katika **Walawi 20:7-8**, ***"Jitakaseni basi, iweni watakatifu, kwa kuwa mimi ndimi BWANA, Mungu wenu. Nanyi zishikeni sheria zangu, na kuzitenda; Mimi ndimi BWANA niwatakasaye ninyi."***

Kutoka kwa hizi aya, wengine wamejitengenezea jina:
YAHWEH QADASH, BWANA AWATAKASAYE.

Mungu ndiye atutakasaye! Ametuhatimisha tufananishwe na mfano wa Mwana Wake. **Yesu Kristo amefanyika utakaso wetu kutoka kwa Mungu** (**1Kor.1:30**) Kanisa linatakaswa katika Kristo Yesu (**1Kor.1:2**). Kwa kufanyika mtu, Yesu alijitolea kwa safari ya utakaso; alikamilishwa kwa njia ya mateso (**Ebr.2:10-11**). Yesu haoni haya kutuita ndugu! Hata hivyo, hii inamaanisha sisi nasi tutateswa katika maisha haya tunapoendelea kutakaswa (**v.12-13**).

Yesu alijitakasa ili atakaswe. Hii inamaanisha kuwa alijitenga Mwenyewe kwa mauti ya msalaba kwa ajili ya maovu yetu, ili kweli ikarejeshwe kwetu (**Yoh.17:19**). Yesu akasema katika **Matendo 26:18** kuwa Mataifa ***wanatakaswa kwa imani ndani yake***.

Mungu Baba na Yesu Kristo wanafanya kazi ya utakaso ndani ya maisha ya watakatifu kwa njia ya Roho Mtakatifu, wakiisha takaswa kwa Damu ya Mwana – kondoo, kwa kututakasa katika ukweli wa Neno. Tunatakaswa kwa:

(a) **Kuoshwa kwa *Damu***
(b) **Kuoshwa kwa *Neno***
(c) **Kuoshwa kwa *Roho***

(a) DAMU

Damu ya Yesu Kristo ni kifaa cha kutuosha katika utakaso.
1 Yoh. 1:7 ***"Na damu yake Yesu, Mwana Wake, yatusafisha dhambi yote."***
1 Yoh. 1:9 ***"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."***
Ebr. 10:22 ***"Na tukaribie wenye moyo wa kweli kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi."***
Ufu. 1:5 ***"Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake."***
Kwa hivyo tumeoshwa kutoka kwa ***kila hatia, aibu na hukumu.***

(b) NENO

Yoh. 17:17 ***"Uwatakase kwa ile kweli; Neno lako ndiyo kweli."***
Yesu Kristo alijitolea kwa ajili ya Kanisa ***"ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno."*** **Efe. 5:26**
Ebr 10:22 ***"hali tumenyunyuziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi.""*** [‘miili yetu inazungumzia ‘*nafsi ya mwili*] ***tunapolipokea Neno, tunaoshwa.***
Yoh. 15:3 ***"Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile Neno nililowaambia."***
Hili ni Neno ‘*rhema*’ au Neno lililo huishwa tunapolisikia tukilisoma ama kulisikia Neno‘*logos*’, ambalo limeandikwa.
Zab. 119:11 ***"Neno lako nimelificha ndani ya moyo wangu, nisije nikakutenda dhambi."***

Neno hututenga, hutufanya watakatifu na hutuleta katika “ile nyingine” ambayo ni Mungu. Mungu ni tofauti, Mtakatifu, hachafuliwi na sera za dunia. Mungu anatuamuru ***"tutoke kati yao tukatengwe nao."*** **2 Kor. 6:17**

(c) ROHO MTAKATIFU

1. Anatutakasa sisi Mataifa, **Rum.15:16;**
2. Anatubadilisha kwa mfano wake, **2Kor.3:18;**
3. Anatupatia kupambanua roho (**1Kor.12:10**) na kututenga na roho zingine;
4. Anafanya kazi ndani yetu ya utakatifu, **1Pet1:2**;
5. Anaweka sheria ndani ya nia zetu na kuziandika ndani ya miyo yetu (**Yer 31:31-34**);
6. Anatuongoza katika kweli yote, **Yoh.16:13.**

AGANO JIPYA

"***Agano Jipya'*** ambalo linazungumziwa katika Yeremia pia limenukuliwa katika **Ebr. 8:8-13.** Maneno haya yanatuonyesha kwamba Roho Mtakatifu huandika Neno la Mungu katika mioyo yetu na kuliweka Neno la Mungu katika akili zetu. Waaminio wanafananishwa na mfano wa Mwana wa Mungu kwa njia ya Roho Mtakatifu na Neno linalofanya kazi ndani yetu. Hii ni kazi ya utakaso, inayotuandaa kutukuzwa ambako tayari amekamilisha kwa ajili yetu. Mungu anatutakasa kwa kusudi hili. Tunapokea hali hii ya kutukuzwa kwa njia ya imani.

KUHESABIWA HAKI NA KUTUKUZWA KATIKA MMOJA

Yesu alikufa msalabani nje ya mji na akafanyika Azazeli kwa ajili ya dhambi za dunia. **Kwa hili tendo tumehesabiwa haki.** Alikuwa pia Mbuzi wa sadaka ambaye damu yake ilipelekwa katika Patakatifu pa watakatifu kwa ajili ya kutukuzwa kwetu.

Kanisa halistahili kubakia tu katika '***ua wa nje'*** palipo na msalaba. *Msalabani,* tunahubiri ujumbe wa wokovu kwa ulimwengu. Kanisa linastahili kupokea ujumbe wa kutukuzwa ili Mwili wa Kristo ukuwe na kutimilika. Kanisa litaweza kuwa na ujasiri kuuhubiri ujumbe wa msalaba tunapopokea utukufu ambao Yesu tayari alitupatia wakati alipofufuka kutoka kwa wafu na akaenda kwenye Kiti cha Rehema mbinguni na damu yake.

1 Kor. 1:18 ***"Kwa sababu Neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuzi, bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu."***

KAZI YA UTAKASO

Tunastahili kuruhusu kazi ya utakaso ifanyike kikamilifu ndani yetu ili tutengwe kabisa kwa ajili ya Mungu. Tumetengwa kwa njia ya Damu ya Yesu; tumetengwa kwa njia ya Roho Mtakatifu na pia tunatengwa kwa ajili ya Neno la Mungu. Neno la Mungu ***"li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo."*** **Ebr.4:12**

NENO LI KAZINI

Kila tunachofanyika ni dhihirisho la Mungu. Tunapofungua vinywa vyetu, Mungu atajilipizia kisasi juu ya maasi yanayotuzunguka (**2Kor.10:6**). Tunapotakaswa kabisa,

Vizuizi vyote ndani yetu vitaondolewa
Ngome zote ndani yetu zitaangushwa
Kila elimu inayojiinua kinyume na elimu ya Kristo itamtii Yesu Kristo

Nguvu kuu za Mungu zitalipiza kisasi juu ya maasi yote karibu nasi. Tunapolihubiri Neno la Mungu kwa watu, Mungu anawashawishi kutubu.

UTIMILIFU WA YESU KRISTO

Ebr. 10:12-14 ***"Lakini huyu alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu; tangu hapo akingojea hata adui zake wawekwe kuwa chini ya miguu yake. Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa."***

Kutukuzwa ni kwa njia ya msalaba. Kwa dhabihu moja, Yesu ametutakasa milele, kwa kumwaga damu yake msalabani. Lakini ilibidi afufuke ili apeleke damu Yake mpaka mbinguni na aiweke kwenye Kiti cha Rehema ili apokee utimilifu wetu.

"Naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele, kwa watu wote wanaomtii, **Ebr.5:9.**

ROHO MTAKATIFU, SHAHIDI KWETU

Ebr.10:19 ***"Basi ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia Patakatifu kwa damu ya Yesu."*** **:22** ***"na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi".***

Hatusita-siti ila tunaukimbilia wokovu. Sasa **tunaukimbilia utimilifu**. Hatuna mashaka juu ya kusamehewa dhambi zetu. Kwa hivyo, **tusiwe na mashaka juu ya kukamilika kwetu** kwa sababu Yule Yesu aliye kufa kwa ajili ya dhambi zetu msalabani, alikufa msalabani kwa ajili ya kutukamilisha. Hallelujah!

KUENDELEA KUKUA KATIKA MAARIFA YA NENO NI MUHIMU KWA AJILI YA MWENENDO WETU

Neno linatuosha tena linatutakasa. ***"Neno lako ni taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu"*** (**Zab.119:105**). Neno ni kiongozi kwa njia ya Roho Mtakatifu ambaye hufunua njia ya Baba.

Filip 2:6-7 yasema kuwa Yesu alijivua Utukufu wake wote akaja duniani. Baada ya kufa na kufufuka tena, Yesu ***"aliketi chini kwenye mkoni wa kuume wa Mungu"*** **(Ebr.10:12).** Alirudi nyumbani kwake mbinguni na mwili uliotukuka. Atarudi tena hapa duniani katika utukufu wake wote na tutakapomuona tutabadilishwa, tukiupokea mwili wa utukufu pia.

TUNAENDELEA KUTAKASWA

Tunapozidi kuruhusu kazi ta utakaso kwa njia ya Damu, Neno na Roho kutenda kazi ndani yetu, ndivyo tutazidi kukabiliana na vitu visivyo takatifu.

Tunatarajio na thibitisho tofauti

(i) Kwa dhabihu moja amenitakasa milele. ***Ninaendelea kutakaswa***.

(ii) Ninairuhusu Damu ya Yesu kunyunyizwa kwa moyo wangu na ***kuniosha kutoka kwa dhambi***.

(iii) ***Neno linafanya kazi ndani yangu*** kila siku, likifichua mawazo yangu na makusudi, likiniosha, likinifanya mtakatifu, na kunifanya zaidi na zaidi kama Yesu.

(iv) Roho wa Mungu – **Roho Mtakatifu -** ***ana nguvu juu yangu*** na ananifanya kuzijua zaidi amri za Mungu.

"Kisha kuna watatu washuhudiao duniani: Roho, na maji, na damu. Na hawa watatu hupatana kwa habari moja," **1Yoh.5:8. Maji ni Neno!**

KUKIRI KWA IMANI

Ebr. 10:22 ***"na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani"***.

Tunaamini na kupokea msamaha na kufanyika kuwa haki katika ua wa nje. Yesu alisulubiwa nje ya mji. Aliipeleka damu yake mpaka Mahali Patakatifu Sana **(Ebr.9:11),** ambapo tunakuja kwa ujasiri kuupokea ule utimilivu ambao tayari ameukamilisha kwa ajili yetu.

Kwa njia ya maziwa ya Neno tunajua wokovu.

Kwa njia ya chakula kigumu cha Neno twajua kuwa tunatukuzwa, na tunajua kuwa tunapokea ukamilifu katika kutakaswa.

KATIKA UTAKASO TUNAUFIKIA UTIMILIFU

Ebr. 5:14 ***"Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima, ambao akili zao, kwa kutumiwa, zimezoezwa kupambanua mema na mabaya."***

Tumeitwa ili tukamilike, wapendwa waliokamilika wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye ndiye Mzaliwa wa Kwanza miongoni mwa ndugu wengi.

SURA YA 3

KUTAKASWA KWA DAMU

KUOSHWA KUTOKANA NA KAZI ZIZIZO NA UHAI – NGUVU ZA UTAKASO KATIKA DAMU

Damu ya Yesu, Mwana-Kondoo wa Mungu aliyemwaga Damu yake kwa ajili ya ondoleo la dhambi zetu, anatutakasa.

DAMU KWA ONDOLEO

Ebr.9:22 ***"Na katika torati, karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na paipo kumwaga damu hakuna ondoleo la dhambi."*** Umwagikaji wa damu kwa ajili ya ondoleo la dhambi ni funzo katika Maandiko Matakatifu kutoka **Mwanzo 3** wakati Mungu alipomchinja mnyama na kuwafanyizia mavazi Adamu na Hawa. Katika sheria ya Musa mambo yote ya sadaka yanatimizwa ndani ya Yesu Kristo msalabani. Umwagikaji wa damu kwa ajili ya ondoleo la dhambi ni kanuni ya zamani katika Neno la Mungu.

Katika somo hili tunatafuta kuelewa jinsi damu invyotuosha.
[Funzo la ukombozi katika damu ya Yesu Kristo limetangulizwa katika somo *'Hadithi ya ukombozi'* katika kitabu *'Utukufu wa Bwana Utafunuliwa.*]
Maandiko ya muhimu katika somo hili yanatoka katika kitabu cha Waebrania.

DAMU INASAFISHA DHAMIRI

Ebr.9:13-14 ***"Kwa maana ikiwa damu ya mbuzi na mafahali na majivu ya ndama ya ng'ombe waliyonyunyiziwa wenye uchafu hutakasa hata kuusafisha mwili, basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?"*** Damu **itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu**, kwamba, inatusafisha kutoka kwa ***hatia, aibu na hukumu.*** **Rum.1:9** inazungumzia jinsi ya kumtumikia Mungu aliye hai kwa roho yetu. Tunaweza kumtumikia Mungu kwa roho zetu kwa sababu damu ya Kristo imesafisha dhamiri yetu [sehemu ya roho ya mtu] na nafsi imeoshwa pia kutoka kwa dhambi.

Ebr.10:22 ***"na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali umenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi".*** Mioyo yetu imenyunyiziwa damu. Tambua yakuwa, katika torati, damu ilinyunyizwa juu ya vyombo vyote katika hema. **Ebr.12:24** inazungumzia ***"damu ya kunyunyizwa"***; tumebatizwa [oshwa] katika maji; tunabatizwa katika Roho Mtakatifu; mioyo yetu inanyunyiziwa damu.

DAMU INAKAMILISHA

Ebr.10:14 ***"Maana kwa toleo moja, amewakamilisha hata milele hao wanaotakswa."***
Toleo ni Yesu Kristo, sana sana damu Yake iliyomwagika. Ametutakasa milele wakati alipopaa kwenda kwa Baba Yake (**Yoh.20:17**) na kuiweka damu Yake kwenye Kiti cha Rehema (**Ebr.9:11-12**). Tunahesabiwa haki pale Msalabani! Ukamilifu wetu ulihakikishiwa wakati Yesu alipoingia utukufuni na damu Yake. ***Tunaendelea kutakaswa*** tunapotembea na Mungu katika safari ya kutoka msalabani hadi utukufuni.

DAMU INAENDELEA KUTUTAKASA

1 Yoh.1:7 ***"Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana Wake, yatusafisha dhambi yote."***
1 Yoh.1:9 ***"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni Mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."*** Tunajufunza funzo la utakaso kwa sababu Neno la Mungu linatufundisha kuwa safari kutoka Msalabani [kuhesabiwa haki] hadi utukufuni [kutimilika] ni kwa njia ya utakaso. Tunaendelea kutakaswa, yaani kutengwa kwa njia ya damu ya Kristo.

KUMWAGIKA KWA DAMU YA KWANZA

Katika **Mwanzo 2-3** twasoma hadithi ya Adamu na Hawa. Waliumbwa bila mawaa yo yote na hatia na waliufurahia uhusiano wao wa ajabu na Mungu. Mungu aliwaonya Adamu na Hawa kwamba wasile matunda kutoka kwa mti wa maarifa ya kujua mema na mabaya. Waliukubali ujanja wa shetani na kuasi maagizo ya Mungu. Matokeo ya dhambi yao ilikuwa ni ***kutenganishwa kutoka kwa Mungu,*** ambao ni kinyume cha utakaso. Njia ya pekee ambapo dhambi yao ingefunikwa ni kumwaga damu.

Mwa.3:21 ***"Bwana Mungu akawafanyia Adamu na Hawa mavazi ya ngozi, akawavika."*** Mungu alimchinja mnyama. Pia aliimwaga damu kwa ajili ya upatanisho. Alimwaga damu ili aifunike dhambi yao. **Umwagikaji wa damu uliifunika dhambi;** kisha akawatengenezea mavazi ya ngozi. Hii ndiyo **dhabihu ya kwanza ya damu kuifunika dhambi ya mwanadamu**.

Adamu na Hawa waliamini kile ambacho Mungu alikuwa amewaambia kuhusu kuja kwa Mwokozi kwa hivyo waliokolewa kwa njia ya imani [walimuamini Mungu]. Mungu akaimwaga damu kuiondoa dhambi yao na akawavika na haki. Umwagikaji wa damu ***uliwatakasa***, [ukiwatenga kwa ajili ya Mungu].

KUFUNIKWA DHAMBI

Ukamilifu wa Mungu ulidhihirika kabla ya mwongo wa gharika. Mungu aliacha uwepo wake duniani; aliiacha njia ambayo mwanadamu angekuja kwake ili amuabudu. **Mwa.3:24** inasema katika mlango wa mashariki wa Adeni kulikuwa na Makerubi waliolinda njia ya mti wa uzima. Pia kulikuwa na upanga wa moto uliogeuka huko na huko. Katika Maandiko Matakatifu, moto pia unawakilisha uwepo wa Mungu ambao unadhihirishwa kwa njia ya Roho Mtakatifu na upanga unawakilisha Neno la Mungu. Mungu alimpa mwanadamu njia ya kumrudia baada ya kufukuzwa kutoka bustanini.

Habili alijua jinsi ya kuleta wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona kama sadaka inayokubalika na Mungu. Kaini alileta sadaka ya matunda, kazi ya mikono yake. Mungu akamwambia Kaini, ***"sadaka yako haikubaliwi"*** (**Mwa.4:5**). Bali akamwambia Habili ***"sadaka yako inakubalika"*** (**a.4**), kwa sababu ***Habili alimcha Mungu*** na alijua kuwa ili sadaka ikubaliwe na Mungu lazima kuwe na umwagikaji wa damu ya Mwana – kondoo.

NUHU

Mwa.6:8, Nuhu alikuwa **mtu mwenye haki**, ***"alipata neema machoni pa BWANA".*** Neema ni kipawa cha Mungu kinachotuwezesha kuamini (**Efe.2:8**). Nuhu alipokea neema hii na akamuamini Mungu. Biblia inatwambia Nuhu alikuwa mtu mwenye haki, bila lawama mbele za Mungu, kwa sababu Nuhu alikuwa mtu aliyeamini yale Mungu alimwambia. Wakati Nuhu alipokuwa akiijenga Safina, Mungu alimwambia Nuhu kuchukuwa wanyama wawili wawili wa kila aina, wanyama na ndege, lakini katika **Mwa.7:2-3** anaambiwa ***"katika wanyama wote walio safi ujitwalie saba saba"***. Hawa walikuwa wa sadaka! Nuhu alikuwa mtu mwenye haki

na alizijua njia za Mungu. Alielewa kufunikwa kwa dhambi, kuwa **hakuna ondoleo la dhambi pasipo umwagikaji wa damu**.
Nuhu kwa kutii alichukuwa wanyama walio safi, halafu katika **Mwa.8:20**, twasoma kuwa Nuhu alifanya hivyo. Wakati mafuriko yalipoisha na Safina ikaingia katika nchi kavu, jambo la kwanza mtu huyu wa haki alifanya lilikuwa ni kutoa dhabihu. Hili lilimpendeza Mungu, na Nuhu na jamii yake wakatakaswa.
Mwa.8:21 ***"BWANA akasikia harufu ya kumridhisha; BWANA akasema moyoni Sitailaani nchi tena baada ya hayo kwa sababu ya wanadamu, maana mawazo ya moyo wa mwanadamu ni mabaya tangu ujana wake; wala sitapiga tena baada ya hao kila kilicho hai kama vile nilivyofanya."***

BIBLIA NI KITABU CHA UKOMBOZI

Jina ambalo limetumiwa sana katika kitabu cha Ufunuo kumaanisha Yesu ni MWANA – kONDOO. Katika **Yoh. 1:29**, Yohana alipasa sauti akisema ***"tazameni Mwana – Kondoo wa Mungu azichukuaye dhambi za dunia"***. Sisi tumetengewa Mungu na Yesu Kristo ***"kwa kutuosha kutoka kwa dhambi kwa Damu yake."*** **Ufu.1:5**.

PASAKA

Kutoka 12 yatwambia hadithi ya Pasaka. Watu wa Israeli walikuwa wakombolewe kutoka katika nyumba ya Mmisri kwa uongozi wa Musa. Musa aliwaambia watu wa Mungu wachukuwe Mwana-kondoo kwa kila nyumba na wamwage damu yake wapake milangoni. Malaika wa kifo alitumwa na Mungu na kila nyumba ambayo haikuwa na alama ya damu mzaliwa wake wa kwanza na wa kila mnyama angekufa, lakini kila makaazi yaliyokuwa na alama ya damu **ingepitwa juu** (**Kutoka.12:12-13**). **Walitakaswa kwa damu**, walitengwa na uovu; wakatengewa utukufu wa Mungu.

AGANO LA SHERIA

Kutoka 24: Mungu alianzisha Agano la Kale, au Agano la Sheria. Musa alikuwa tayari amepokea Sheria katika vibao vya mawe na sasa kusanyiko lote lilikusanyika na Wazee, akawasomea wote maneno yote ya Sheria ambayo Mungu alinena. Watu wote wakaitikia, *"Maneno yote aliyoyanena BWANA tutayatenda"* (**a.3**). Kisha Musa akajenga madhabahu ambayo alinyunyizia damu. Pia akawanyunyizia watu damu. Kila mtu alinyunyiziwa damu na madhabahu pia. Kunyunyiza damu kuliwatakasa watu na madhabahu.

Baada ya Agano la Damu…
v.9-11 ***"Ndipo akakwea juu, Musa na Haruni, na Nadabu, na Abihu, na watu sabini miongoni mwa wazee wa Israeli; wakamwona Mungu wa Israeli; chini ya miguu yakepalikuwa na kama sakafu iliyofanyiswa kwa yakuti samawi, kama zile mbingu zenyewe kwa usafi wake. Naye hakuweka mkono wake juu ya hao wakuu wa wana wa Israeli; nao wakamwona Mungu, wakala na kunywa."***Hakuweka mkono wake juu yao ***kwa sababu walikuwa wamefunikwa kwa damu***, kwa hivyo waliweza kuingia katika uwepo wa Mungu Mwenyezi na kumuona Mungu wa Israeli Mwenyewe na hawakufa; wakala na kunywa Naye. Kwa sababu damu iliwafunika, damu iliwatakasa; halafu waliweza kuingia katika utukufu!

SADAKA YA SIKU BAADA YA SIKU

Kutoka 29:38-46 inaelezea jinsi sadaka ya siku baada siku ilivyostahili kuwa: **Mwana - kondoo, ambaye damu yake ilimwagwa, na kutolewa kwa Mungu kama sadaka ya kusongezwa; huyu Mwana – Kondoo aliteketezwa kabisa.**

Tena pamoja na Mwana-Kondoo kulikuwa na sadaka ya Unga mzuri uliochanganywa na mafuta yenye kupondwa, asubuhi na jioni. Usiku aliotwaliwa, Yesu alitwaa sadaka ya Unga Mzuri, ambao ulikuwa mkate na akasema huu ni ***'Mwili Wangu'***. Alichukua sadaka ya divai na akasema,***'hii ni Damu Yangu tena mimi ni Mwana-Kondoo wa sadaka ya kuteketezwa'***. Yesu aliitimiza torati. Tunamkumbuka mara kwa mara tunaposhiriki katika Meza ya Bwana, tunapojitenga kwa ajili Yake. Sadaka ya kila siku inatimizwa katika **kushiriki Meza ya Bwana ambayo inatutakasa maisha yetu.**

TUNAOSHWA KWA MWILI NA DAMU YA YESU KRISTO

1. <u>TUNAOSHWA KWA MWILI WAKE</u>

Katika **Ebr.10:4-10** tunaona kwamba **tunatakaswa, kwa njia ya dhabihu moja ya Yesu Kristo**. Yesu Kristo alikuja ulimwenguni kutimiza mapenzi makamilifu ya Mungu, ***"Tazama nimekuja – katika gombo la chuo nimeandikiwa – nifanye mapenzi yako, Mungu"*** **a7.** Kwa kujitolea msalabani, Yesu alitimiza sheria ya Agano la Kale inayohusu sadaka na sadaka za kuteketezwa na pia ***"aliondoa la kwanza kusudi alisimamishe la pili"*** **a9.** Kujitoa kwake Yesu kulitimiza mapenzi ya Mungu. ***"Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi."*** **a. 4.**

Hii inawezekana ***"Kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu."*** **a.10**, tumepata utakaso, tumetengwa kusudi mapenzi ya Mungu yatimie ndani yetu. Mapenzi ya Mungu ni ***"utakaso wetu"*** (**1 Thess.4:3**), hivyo ni kusema, ***"jinsi iwapasavyo kuenenda na kumpendeza Mungu"*** (**1 Thess.4:2**). Kitabu cha **Warumi 12:1-2** kinatufundisha jinsi ya kujitenga kwa ajili ya Mungu kwa **<u>kuitoa miili yetu</u>**, ambayo inawezekana kwa ajili ya Yesu kujitoa mwili wake, tunafanywa upya nia zetu na kuingia katika kufahamu mapenzi ya Mungu. Mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kupendeza na makamilifu yanafunuliwa na tunaingia katika kutimizwa kwake – mapenzi yale ambayo Yesu pia alitimiza. Hii ni kazi ya utakaso ambayo imeletwa kwa njia ya Yesu kujitoa kama dhabihu msalabani.

2. <u>TUNAOSHWA KWA DAMU YAKE</u>

Ebr.10:19-25 Kristo aliingia Patakatifu kwa damu Yake Mwenyewe mara moja kwa wote kupeana ukombozi wa dhambi zetu, na ***"njia ile aliyotuanzia iliyo mpya, iliyo hai, ipitayo katika pazia, yaani, mwili wake"*** **a20**. Kwa sababu ya damu Yake katika Patakatifu na kwa sababu Yeye ni ***"Kuhani Mkuu juu ya nyumba ya Mungu"*** **a21**, tunawezeshwa kuenenda katika utakatifu. Tunawezeshwa ***"kukaribia wenye moyo wa kweli kwa utimilifu wa imani"*** **a22**. Na kuweza "***kulishika sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke; maana yake aliyeahidi ni Mwaminifu."*** **a23**. ***"Tuangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri"*** **a24**. ***"Wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo Siku ile kuwa inakaribia."*** **a25**.

Ebr.13:12 ***"Kwa ajili hii, Yesu naye aliwatakasa watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango."*** Tunatakaswa kwa damu yake, ambayo inatutenga, kutoka kwa dhambi nakutufanya tumuelekee Mungu, ikituwezesha kuenenda katika ***"njia mpya iliyo hai"***. Kwa hivyo anasema, ***"tokeni kati yao na mjitenge, asema Bwana. Msiguze cho chote kilicho kiovu, name nitawapokea."*** **2Kor.6:17**.

MUNGU ANAFANYA KAZI NDANI YETU KWA SABABU TUMETENGWA KWA DAMU

Ebr.13:20-21 ***"Basi Mungu wa amani aliyemleta tena kutoka kwa wafu, Mchungaji Mkuu wa Kondoo, kwa damu ya Agano la milele, yeye Bwana wetu Yesu, awafanye ninyi kuwa***

wakamilifu katika kila tendo jema, mpate kuyafanya mapenzi yake, naye akifanya ndani yetu lipendezalo mbele zake, kwa Yesu Kristo; utukufu una Yeye milele na milele. Amina."

1. Kupitia kwa damu ya Agano la milele, Mungu anafanya kazi ndani yetu.
2. Atawafanya ninyi kuwa wakamilifu katika kila tendo jema, mpate kuyafanya mapenzi yake

SISI NI KAZI YA MIKONO YAKE

Efe.2:10 ***"Maana tu kazi ya mikono yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo."*** Yesu Kristo alitutakasa kwa damu ya Agano la milele tuenende katika matendo mema ambayo alitangulia kututengenezea mbeleni.
Ni kwa njia ya damu ya agano la milele linalomuwezesha Mungu kuifanya kazi hiyo kikamilifu katika maisha yetu kuikamilisha kazi hiyo.

MUNGU ANATUCHAGUA NA AMETOA DAMU ILI ITUTAKASE

1Pet.1:2 ***"Kama vile Mungu Baba alivyotangulia kuwajua katika kutakaswa na Roho, hata mpate kutii na kunyunyiziwa damu ya Kristo."*** Tumechaguliwa; tumeteuliwa kulingana na vile Mungu alivyotangulia kutujua. Tumeteuliwa kukamilishwa katika utakaso kwa Roho, ili kazi ya nguvu zilizomo katika damu ili tutengwe kutokana na dhambi.

MUNGU NI MTAKATIFU NA ANATAKA TUWE WATAKATIFU [TUOSHWE KABISA]

1Pet.1:15-16 ***"Basi kama yeye aliyewaita ni Mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote; kwa maana imeandikwa Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni Mtakatifu.'"*** Tumeitwa tuwe watakatifu. Hii inawezekana kwa sababu ya nguvu za ukombozi zilizomo katika utakaso wa damu; kunyunyiziwa kwa damu inayotuosha.

Ebr.7:26 ***Maana ilitupasa sisi tuwe na Kuhani Mkuu wa namna hii aliye mtakatifu, asiyekuwa na uovu, asiyekuwa na waa lo lote, aliyetengwa na wakosaji, aliyekuwa juu kuliko mbingu."*** Kuhanu wetu Mkuu ni Mtakatifu na anatutakasa.

TUMEOSHWA KWA DAMU ILI TUINGIE UTUKUFUNI KAMA WAFALME NA MAKUHANI

Ufu.1:5 ***"Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu Yake."*** Yesu Kristo alituosha kutoka kwa dhambi zetu kwa damu yake Mwenyewe. **a.6** ***"na kutufanya kuwa wafalme na makuhani kwa Mungu, naye ni Baba Yake; utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele. Amina."*** Ametufanya kuwa wafalme na makuhani kwa Mungu na Baba Yake. Wafalme wanabeba utukufu. Mungu ametuosha kwa damu ili tuweze kuingia utukufuni! Hallelujah! Bila damu hatungeweza kuingia utukufuni!

SURA YA 4

KUTAKASWA KWA NENO

KUANDAA KANISA LA UTUKUFU – KUOSHWA KATIKA NGUVU ZA NENO

Mstari mkuu katika funzo hili ni **Efe. 5:26**, ukizungumzia juu ya Kristo baada ya kulipenda Kanisa na kujitoa Mwenyewe kwa ajili yake, ***"ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika Neno."*** **a.26** inatwambia kuwa ***"Kristo alilipenda Kanisa hata akajitoa kwa ajili yake".*** Hii inazungumzia juu ya kifo chake kwa ajili yetu; kifo chake, yaani kuimwaga damu Yake, imetuosha kama vile tumeona katika funzo lililo malizika. Bali pia, kufa Kwake na kufufuka kulimpa uwezo wa kutuosha na kututakasa kanisa kwa maji katika Neno. Pasipo kifo chake Yesu, Neno halingeweza kututakasa na kutusafisha. Tunastahili kuokoka kwa imani katika damu ya Yesu Kristo ituoshayo kutokana na dhambi yote. Tunapo okoka, Neno linaanza kufanya kazi ndani yetu katika kutusafisha likituleta katika hali ya utimilifu wa utukufu, ***"lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa,"*** (**Efe.5:27**). Lengo la Mungu katika historia ya ukombozi ni Kanisa tukufu kwa ajili ya Mwana Wake. Mungu hashindwi katika kuyaafikia makusudi yake, maana tayari yamekamilishwa katika Kristo Yesu (**Efe.3:11**).

Yesu anakusudia kujitwalia Kanisa tukufu. Hili Kanisa linatakaswa na kuoshwa. Ni Yesu mwenyewe ndiye anayeliosha na kulitakasa kwa kuliosha na maji ya Neno. Mambo mawili yanatendeka: Yesu [ambaye ndiye Neno, **Yoh.1:1**] anasema kuwa Neno lake linatutakasa na kutuosha pia. Jinsi tu maji yanavyotuosha na kuwa safi, Neno la Mungu linatuosha na kututakasa nafsi zetu. Utakaso wa nafsi unahusisha kubadilika kutoka katika upeo wa hisia hadi upeo wa roho, yaani, nia yetu, maamuzi na hisia zetu na kuanza kutafuta yale yaliyo ya juu, (**Kol.3:1-2**).

AMINI KWELI:
2 Thess.2:13 ***"Lakini imetupasa sisi kumshukuru Mungu siku zote kwa ajili yenu, ndugu mliopendwa na Bwana, kwa kuwa Mungu amewachagua tangu mwanzo mpate wokovu, katika kutakaswa na Roho na kuamini Kweli."***
Unapoanza kuiamini kweli na sio uongo tena unatakaswa na lile Neno ambalo umeamini. Yesu anatuombea katika **Yoh.17:17** ***"Uwatakase kwa ile kweli. Neno lako ndiyo kweli."*** Ni ukweli wa Neno la Mungu ndio unaotuweka huru kutokana na kuamini uongo. Ni wale tu waliozaliwa na Roho ndio wanaoweza kulipokea Neno la Mungu kwa sababu linapambanuliwa kwa Roho, **1 Kor.2:14**. Yesu alisema ***"kweli itawaweka huru"***, **Yoh.8:32**. Kuamini ukweli huleta uhuru.

Mwandishi wa Zaburi aliandika ***"kufafanusha kwa maneno Yako kwatia nuru."*** **(Zab.119:130**). Tunapoliamini Neno la Mungu tunahamishwa kutoka katika ufalme wa giza na kutuingiza katika Ufalme wake Bwana Wetu Yesu Kristo, (**Kol.1:13**). Huu ni mfano wa ajabu wa utakaso: kutengwa kwa ajili ya kuiamini kweli.

TUMEOSHWA KWA MAJI SAFI:
Ebr.10:22 ***"Na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbya, yumeoshwa miili kwa maji safi."*** Hakika hili halizungumzii kuoga kwa mwili wa asili. Hili linazungumzia nafsi ya mtu ambayo ndiyo inayooshwa, kutuwezesha kukaribia Mungu na kutuandaa kwa ajili ya kuupokea utukufu. Maji safi yanayotuosha ni Neno la Mungu. Mwandishi wa Zaburi anasema, ***"Maneno ya BWANA ni***

maneno safi," (**Zab.12:6**); maneno ya Bwana yanasafisha na kututakasa ndani, kuosha nafsi zetu.

NENO LA MUNGU HUZIGAWANYA NAFSI NA ROHO:
Ebr.4:12 ***"Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.""***
Kazi ya kwanza kuu ambayo Neno la Mungu linafanya ni kugawa roho na nafsi. Hiyo kazi ni muhimu kwa utakaso ambao hutendeka tu kwa njia ya kulipokea Neno la Mungu. Hakuna dini nyingine au filosofia, thiologia au elimu nyingine yo yote inayofundisha au kujua jinsi nafsi na roho zinavyogawanyika, ila hii ndiyo njia ya pekee ambayo nafsi inatakaswa kabisa. Neno la Mungu linaleta uponyaji na uhuisho kwa nafsi, kwa kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. Mtu wa roho anayatambua mawazo ya roho na mawazo ya nafsi. Nafsi inahitaji urejesho kama sehemu ambayo imejitolea ya mtu wa roho ambaye Mungu ameumba katika mfano na sura Yake.

MAUNGAMO YETU NI KUTAFAKARI KWETU:
Ebr.4:14 ***"Basi, iwapo tunae Kuhani Mkuu aliyeingia ndani katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu na tuyashike sana maungamo yetu."***
Maungamo yetu ni kile tuachoamini kuhusiana na Neno la Mungu, na tunatakikana kutafakari juu ya Neno la Mungu siku zote. Maungamo na tafakari za aina hii zinatubadilisha, kuleta ***kufaulu na mafanikio*** katika safari yetu na Mungu.

Tafakari juu ya Neno la Mungu
Yoshua 1:7-8 ***"Uwe hodari tu na ushujaa mwingi, uangalie kutenda sawa sawa na sheria yote aliyokuamuru Musa mtumishi wangu, usiiache, kwenda mkono wa kuume au wa kushoto , upate kufanikiwa sana kila uendako. Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake, mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawa sawa na maneno yote yaliyoandikwa humo,; maana ndipo utakapoifanikisha njia yako."***

Zab.119:97 ***"Sheria yako naipenda mno ajabu, ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa."***

Zab.119:148 ***"Macho yangu yalitangulia makesha ya usiku, ili kuitafakari ahadi Yako."***
Wakati tunapolitafakari Neno la Mungu, huwa linazama ndani yetu, na kuanza kuifanya kazi ya kutuosha na kutusafisha.

KUJIFUNZA NENO KATIKA ZABURI 119

Zab. 119:11 ***"Moyoni mwangu nimeliweka Neno lako, nisije nikakutenda dhambi."*** Lifiche Neno moyoni wako na hutatenda dhambi.

Zab.119:25 ***"Unihuishe sawa sawa na Neno lako."*** ***Zab*** **119:107** ***"Nimeteswa mno, Ee Bwana unihuishe sawa sawa na Neno lako."*** Neno linatuhuisha.

Zab.119:28 ***"Nafsi yangu imeyeyuka kwa uzito, unitie nguvu sawa sawa na Neno lako."***
Neno linatutia nguvu.

Zab.119:38 ***"umthibitishie mtumishi wako ahadi yako, inayohusu kicho chako."***
Neno linatuthibitisha ndani ya Bwana.

Zab.119:42 ***Nami nitamujibu Neno alinilaumuye, kwa maana nalitumainia Neno Lako."***
Neno ni neno la Kutumainiwa.

Zab.119:43 ***"Usiliondoe Neno la kweli kinywani mwangu kamwe, maana nimezingojea hukumu zako."*** Neno ni neno la kweli.

Zab.119:50 ***"Hii ndiyo faraja yangu katika taabu yangu, ya kwamba ahadi yako imenihuisha."*** Neno lina tufariji, na kuleta Uzima.

Zab.119:57-58 ***"Bwana ndiye aliye fungu langu, nimesema kwamba nitayatii meneno yake. Nimekuomba radhi kwa moyo wangu wote, unifadhili sawa sawa na ahadi yako."*** Bwana anarehemu sawa sawa na Neno Lake.

Zab.119:65 ***"Umemtendea mema mtumishi wako, Ee Bwana, sawa sawa na Neno Lako."*** Bwana atatutendea mema sisi kulingana na Neno Lake.

Zab.119:67 ***"Kabla sijateswa mimi nalipotea, lakini sasa nimelitii Neno Lako."*** Niliteswa wakati nilipopotea. Nikilitii Neno Lako sitapotea.

Zab.119:74 ***Wakuchao na wanione na kufurahi, kwa sababu nimelingojea Neno Lako."*** [pia **Zab.119:81, 114, 147**]. Kuna matumaini katika Neno Lake.

Zab.119:89 ***"Ee, Bwana, Neno Lako lasimama imara mbinguni hata milele."*** Neno la Mungu halibadiliki.

Zab.119:101 ***"Nimeiepusha miguu yangu na kila njia mbaya, ili nilitii Neno Lako."*** Siri ni kuliweka Neno la Mungu.

Zab.119:103 ***"Mausia yako ni matamu sana kupita asali kinywani mwangu."*** Neno ni tamu.

YESU NI NENO: AMENENA
Ebr.1:1-2 ***"Mungu ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemuweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu."***

Yoh.1:1 ***"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu."***
a.14 ***"Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli."***
Yesu ni Neno. Mungu amenena katika Mwana.

NIA ZETU ZINAGEUZWA NA KUFANYWA UPYA KWA NENO

Rum.12:2 ***"Wala msiifwatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema ya kumpendeza na ukamilifu."*** Kazi ya utakaso wa Neno inatufanya upya nia zetu na kutugeuza kuyajua mapenzi ya Mungu.
Efe.4:23 ***"na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu."***

Efe.4:24 ***"mkavae mtu mpya, ulioumbwa kwa nama ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli."*** Sehemu ya mtu mpya ni kuwa na roho ya nia iliyofanywa upya.

Efe.4:21 ***"ikiwa mlimsikia mkafundishwa katika yeye, kama kweli ilivyo katika Yesu."*** Ukweli unatushawishi kujitenga na mwili na kuvaa nia iliyo mpya, ambayo ni sehemu ya mtu mpya.

2 Kor.10:5 ***"tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuwacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikra ipate kumtii Kristo."*** Hii inamaanisha kuteka nyara kila wazo na kila kitu kijiinuwacho katika nia zetu kinyume na Neno la Mungu, yaani, '*kutii'* Neno

la Mungu, kukabiliana na kila wazo na ngome katika nia zetu kulingana na maarifa ya Neno la Mungu.
Kazi ya utakaso kwa Neno hugeuza na kufanya upya nia zetu, matokeo yakiwa kwamba tunatengwa kuyajua mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na makamilifu. (**Rum.12:2**).

NENO LINATUOSHA
Yoh. 15:3 ***"ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile Neno nililowaambia."*** Yesu alisema tumekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile Neno alilotwambia. Hii ni kazi ya utakaso, ambayo inatutenga kwa ajili ya Mungu, kukaa ndani ya mzabibu, kuzaa matunda mengi, na kwa hivyo kumtukuza Mungu. Utakaso huleta utukufu; kazi inayoendelea ya utakaso inadhihirika wakati tunapozaa matunda mengi. Kule kuzaa matunda mengi kunadhihirisha utukufu wa Baba.

Yesu hana kitengo cha watoto wasiozaa matunda; kila tawi lisilozaa hulinganishwa na lile tawi liliokufa au kauka; ambalo hukatwa na kutupwa motoni; Kisha matawi yanayozaa husafishwa: ***hii ni kazi ya utakaso***. Neno *rhema* ambalo ni [Neno lililohuishwa, Neno la imani ambalo ni lazima tulitii], ni mbegu izaayo matunda. Katika **Matendo 18**, Paulo kwa haraka angeondoka katika maeneo ya Korintho kwa sababu ya upinzani na mateso, lakini Bwana akamzungumzia [Neno la rhema], na akamwambia akae Korintho, akinena Neno la Mungu. Bwana alimwahidi matunda mengi na watu wengi wakaokoka katika mji huo (**Matendo 18:6-11**). Neno la Mungu lilimtenga Paulo kwa ajili ya kutii Mungu kule Korintho.

NENO LILE LILILOPANDWA NDANI

Yakobo 1:21 ***"kwa hiyo wekeeni mbali uchafu wote na ubaya uzidio, na kupokea kwa upole Neno lile lililopandwa ndani, liwezalo kuziokoa roho zenu."***
Tuweke mbali kila tendo la mwili, natupokee Neno ambalo litaweza kuokoa nafsi Zetu.
1 Thess.1:6 ***"Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana, mkiisha lipokea Neno kwa dhiki nyingi, pamoja na raha ya Roho Mtakatifu."*** Wakati umo katika dhiki nyingi Neno litakuja na kukuokoa.

1 Pet.1:22-25 ***"mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kutii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo. Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili si kwa mbegu iharibikayo bali kwa hiyo isiyoharibika; kwa Neno la Mungu lenye Uzima, lidumulo hata milele. Maana, mwili wote ni kama majani na fahari yake yote ni kama ua la majani. Majani hukauka na ua lake huanguka; bali Neno la Bwana hudmu hata milele. Na Neno hilo ni Neno lile jema lililohubiriwa kwenu."***
Nafsi zetu zinaoshwa kwa ajili ya kutii kweli; kwa njia ya kupokea mbegu ya Neno isiyoharibika. Neno linalohubiriwa linapoingia ndani yetu linatuokoa nafsi zetu. Hili ni Neno ambalo limepandwa ndani.

1 Yoh.3:3 ***"na kila mwenye matumaini haya katika yeye hujitakasa, kama yeye alivyo Mtakatifu."*** Tunajitakasa wenyewe kwa kulisikia Neno na kulitii.

Efe.4:29 ***"Neno lolote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu bali lililo jema la kumfaa menye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia."*** Tukinena Neno safi la Mungu, litajenga na kuwapa neema wasikiao. Kwa hazina iliyomo ndani ya moyo wa mtu, kinywa chake hunena: tunafaa kulipokea Neno lililopandwa ndani ya mioyo yetu. Kisha tunapolinena hilo Neno litatimia.

Mt.24:35 ***"Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe."*** *Neno la Mung li hai na linadumu milele. Linatakiwa liishi ndani yetu*: **Rum.10:8** ***"Lile Neno li karibu nawe katika kinywa chako, na katika moyo wako."***

Kol.3:16 ***"Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa saburi na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimuimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu."*** Neno litawezaje kudumu ndani yetu kwa wingi? Kwanza, tuanatakikana kuwa tumepokea Neno liliilopandwa ndani yetu; Pili, kwa kuziimba saburi na tenzi za rohoni kwa Bwana.

NENO KAZINI

Rum.10:8-9 ***"Lakini yasemaje? 'Lile Neno li karibu nawe, katika kinywa chako, na katika moyo wako, yaani, ni lile Neno la imani tulihubirilo. Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako yakuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka."***

Tunapolisema Neno, Neno la imani ambalo tumelisikia na ambalo tumelipokea katika mioyo yetu, tunaokoka. Hii inamaanisha nini? Hili ni Neno linalofanya kazi, likituosha, likitutenga kwa ajili ya kuamini ile kweli. Tunapolisikia Neno imani inajengeka ndani yetu.

Rum.10:17 ***"Basi imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa kwa Neno la Kristo."***

Kulisikia Neno kulileta muujiza wa uponyaji:

Matendo.14:7-10 ***"Wakakaa huko, wakiihubiri injili. Na huko Listra palikuwa na mtu mmoja dhaifu wa mguu, kiwete tangu tumboni mwa mamaye, ambaye hajaenda kabisa. Mtu huyo alimsikia Paulo akinena ambaye akamkazia macho na kuona yakuwa ana imani ya kuponywa, akasema kwa sauti kuu, simama kwa miguu yako sawa sawa. Akasimama upesi akaenda."***

1. Paulo alihuburi Neno.
2. Kiwete alisikia Neno.
3. Paulo aliona imani ikiingia moyoni mwake.
4. Matokeo ni uponyaji mkuu.

Kulisikia Neno kulileta wokovu:

Matendo.16:14 ***"Mwanamke mmoja, jina lake Lidia mwenye kuuza rangi za zambarau, mwenyeji wa Thiatira, mcha Mungu, akatusikiliza, ambaye moyo wake ulifunguliwa na Bwana, ayatunze maneno yaliyonenwa na Paulo.."***

1. Paulo alihuburi Neno.
2. Lidia alisikia Neno
3. Bwana akaufungua moyo wake na imani ikaingia ndani yake.
4. Aliamini na akaokoka.

<u>Kuamini Neno la Mungu huleta utakaso</u>:
Tunatakaswa kwa kuiamini kweli;
Tunatakaswa kwa kuoshwa kwa maji safi ya Neno;
Nafsi zetu zinaoshwa kwa kutengwa kutoka kwa roho kwa njia ya Neno la Mungu;
Nafsi zetu zinaoshwa kwa kufanywa upya kwa njia ya Neno;
Tunatakaswa kwa kusafishwa tunapolipokea Neno lile linalonenwa;
Tunatakaswa na Neno ambalo limepandwa ndani yetu;
Tunatakaswa na Neno linalifanya kazi ndani yetu.
Nguvu za uwezo wa Neno la Mungu zinatuandaa kwa ajili ya utukufu!

Yesu yuko analiandaa Kanisa kwa ajili ya Utukufu. Alijitoa kwa ajili yetu na sasa anatutakasa na ***"Kutusafisha kwa maji katika Neno,"*** **Efe.5:26.** Kupitia kwa utakaso, Kanisa liko linaandaliwa kwa ajili ya utukufu. Neno la Mungu ndicho kifaa kilicho kikuu kuuleta huo utakaso mkamilifu. Yesu alimuomba Baba katika **Yoh.17:17, *"Uwatakase kwa ile kweli;Neno Lako ndiyo kweli."*** Hakika Neno la Mungu ni ukweli unaotutakasa.

Neno la Mungu linatutakasa!

Neon la Mungu linatuosha!

Neno la Mungu linatusafisha!

Neno la Mungu linatuandaa kwa ajili ya utukufu!

SURA YA 5

KUTAKASWA KWA ROHO

- *nguvu za utakaso za Roho Mtakatifu*.

Roho Mtakatifu wa Mungu anahusika katika kutuleta sisi kwake Yesu Kristo, kutulea katika Kristo mpaka tufananishwe na mfano wake katika utumilifu na kujiletea Kanisa lisilo na mawaa mbele ya uwepo wa utukufu Wake.

ROHO MTAKATIFU ANATUTENGA KWA AJILI YA WOKOVU

2 Thess.2:13 ***"Lakini imetupasa sisi kumshukuru Mungu siku zote kwa ajili yenu, ndugu mliopendwa na Bwana, kwa kuwa Mungu amewachagua tangu mwanzo mpate wokovu, katika kutakaswa na Roho, na kuiamini kweli."***

Wokovu wetu utabainikaje kuwa halali? Bwana ametuchagua kuokoka. Hatuwezi kuokoka hadi Roho Mtakatifu atuvute. Roho Mtakatifu anakuja kututenga kwa ajili ya wokovu. Roho Mtakatifu yu hai duniani akituvuta kwake Mungu. Anakuja mahali palipo na giza kisha anaanza ***"kutulia"*** (**Mwa.1:2**). Roho Mtakatifu anatuleta kwake Yesu!

ROHO MTAKATIFU ANATUFANYA TUKUBALIKE KWA MUNGU

Rum.15:16 ***"…ili niwe mhudumu wa Kristo Yesu kati ya watu wa mataifa, niifanyie Injili ya Mungu kazi ya ukuhani, kusudi mataifa wawe sadaka yenye kibali, ikiisha kutakaswa na Roho Mtakatifu."***

Roho Mtakatifu anatuandaa kuyakubali mapenzi ya Mungu katika maisha yetu, pia kutufanya tukubalike kwa Mungu. Kwa njia Yake yeye kukaa ndani, Mkristo anatakaswa, yaani, anakubalika kwa Mungu.

Katika **Matendo 15:8-9** Petro alikuwa akishuhudia kuhusu yaliyotendeka katika nyumba ya Kornelio, ***"Na Mungu, ajuaye mioyo ya watu, akawashuhudia, kwa kuwapa Roho Mtakatifu vile vile alivyotupa sisi, wala hakufanya tofauti kati yetu sisi na wao, akiwasafisha mioyo yao kwa imani."*** Roho Mtakatifu aliwatenga hawa Mataifa kwa ajili ya wokovu na kisha akaja kwao kuwafanya wakubalike kwa Mungu. Petro mtume alitambua kuwa Mataifa wamekubalika kwa Mungu kwa sababu Roho Mtakatifu aliwashukia.

TUNATAKASWA NDANI YA KRISTO

1 Kor.1:2 ***"Kwa Kanisa la Mungu lililoko Korintho, kwa wale waliotakaswa katika Kristo Yesu."*** 'Kristo' maana yake 'aliyetiwa mafuta'. Yesu alitiwa mafuta na Roho Mtakatifu, (**Lu.4:18, Matendo 10:38**). Tunatakaswa tunapokuwa ndani ya mtiwa mafuta, Kristo Yesu. Tuna zaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu; tunabatizwa katika Kristo (**Gal.3:27**); tunapokea utimilifu katika Roho Mtakatifu kwa njia ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ni Roho Mtakatifu ndiye anayetuhifadhi katika Kristo.

KUTENGWA KUTOKANA NA DHAMBI YA MWILI, KWA AJILI YA MUNGU

1 Kor.6:9-10 inatupatia orodha ya dhambi za mwili ambazo zitatufungia nje katika ufalme wa Mungu. Kisha **a.11** Paulo anasema: *"**Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, lakini mkatakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika Jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu.."*** Kuna vifaa viwili ambavyo hututakasa: Jina la Yesu na Roho wa Mungu. Ni Roho Mtakatifu ndiye anayetutenga kwa ajili ya Mungu. Ni kwa Roho Mtakatifu tunawezeshwa kumjua Yesu kama Bwana, **(1Kor.12:3).** Wale wanaoendelea katika

dhambi za dunia hawataingia katika ufalme wa Mungu. Roho Mtakatifu hataendelea kushindana na wale wanaoendelea kutenda dhambi. (**Mwa.6:3).**

KUTENGWA KWA ROHO MTAKATIFU

1 Pet.1:2 ***"Kama vile Mungu Baba alivyotangulia kuwajua katika kutakaswa na Roho, hata mpate kutii na kunyunyiziwa damu ya Yesu Kristo, neema na amani ziongezwe kwenu."***

Tumechaguliwa, tukatengwa, kwa Roho Mtakatifu. Anaendelea kututakasa kwa kutii na kunyunyiziwa damu ya Yesu Kristo. Roho Mtakatifu anatutenga kwa ajili ya kuitii Injili. Ni kwa njia tu ya Roho Mtakatifu tutaweza kupokea ukweli katika roho uliomo katika damu ya Yesu.

KAZI INAYOENDELEA YA ROHO MTAKATIFU

Tito 3:4-5 *"Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa mwanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa sisi kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya kwa Roho Mtakatifu."*

*'*Kufanywa upya kwa Roho Mtakatifu' ni kazi inayoendelea ya Roho Mtakatifu katika maisha yetu. **2 Cor.4:16** *"...**utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku."***

Roho Mtakatifu anatuleta katika wokovu
Roho Mtakatifu anatutakasa ili tuokoke.
Roho Mtakatifu anatutakasa ili tupate kunyunyiziwa damu.
Roho Mtakatifu anatutakasa ili tuenende katika utii wa Neno la Mungu.
Roho Mtakatifu anatutakasa ili tuendelee kunyunyiziwa damu, kwa kutuosha siku kwa siku na kufanywa upya ndani.

TWAMAANISHA NINI TUNAPOSEMA KUTAKASWA?

Kutakaswa*:- kutukuza, kutengwa, kuweka wakfu, kutawaza, kutenga, takasa, utakatifu; haliya utakatifu kinyume na vitu chafu. Kutakaswa ni kutawazwa. Katika Agano la Kale, wakati kuhani alipokuwa akitawazwa, alitengwa kwa ajili ya Mungu. Kuna mambo ambayo hakustahili kufanya au angekuwa najisi. Katika Agano Jipya Neno linafafanua uthihirisho wa uzima unaotokana na Roho Mtakatifu akaaye ndani.*

ROHO AKAAYE NDANI YETU ANAFANYA MIILI YETU KUWA TAKATIFU

1 Kor.3:16-17 ***"Hamjui kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na yakuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamuharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi."***

Sisi ni hekalu la Mungu na hekalu la Mungu ni takatifu. Tusiliharibu hekalu.

KAZI YA ROHO MTAKATIFU NDANI YETU NI KUTUTAKASA.

Ikiwa kutakaswa ni sawa na mwenendo wetu na kutakaswa ni kuwa watakatifu, waliotengwa, waliotawazwa, Roho Mtakatifu anafanyaje haya ndani yetu?

1. Roho Mtakatifu - Roho Mkamilifu wa Mungu:

Isa.11:2 ***"Na Roho wa BWANA atakaa juu yake, Roho wa hemima na ufahamu, Roho wa shauri na uweza, Roho wa maarifa ya kumcha BWANA."*** Tunapokea kutoka kwa Roho wa Mungu hekima, maarifa na ufahamu, ushauri, uweza na kumcha Bwana. Tunahitaji Roho mkamilivu wa Mungu afanye kazi ndani yetu. Yeye ndiye njia ya utakaso wetu.

2. Roho wa Mungu anatufanya upya nia zetu:

Katika **Efe.4:23** Paulo anatwambia ***"na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu".*** Ni Roho wa Mungu ndiye atufanyaye upya nia zetu. **Rum.12:2** ***"bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kupendeza na ukamilifu."*** Matokeo ya kufanywa upya katika nia zetu ni kujua mapenzi ya Mungu.

3. Roho Mtakatifu anatuletea ufunuo.

Efe.1:17 ***"Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi Roho wa hekima na wa ufunuo katika kumjua Yeye."***

4. Roho Mtakatifu anatusaidia katika safari wetu:-

Ni safari ya imani:

Gal.2:20 ***"Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu."***

Tangu mwanzo hadi mwisho:

Gal.3:3 ***"…Baada ya kuanza katika Roho mnataka kukamilishwa sasa katika mwili?"*** Tumezaliwa ya pili kwa Roho wa Mungu, na ni Roho Mtakatifu ndiye anayekamilisha kazi ya ukamilifu.

Anamuumba Kristo ndani yetu:

Gal.4:19 Paulo anasema ***"Vitoto vyangu, ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu."*** Lengo la safari ya imani ni mfano wa Kristo uumbike ndani yetu. Hii ndiyo kazi Roho anafanya. Ana muumba Kristo ndani yetu. Tunapomtazama Bwana, tunabadilishwa kutoka utukufu hadi utukufu (**2Kor.3:18**).

Anatupatia uhuru:

Gal.5:1 ***"Katika ungwana huo, Kristo alituandika huru, kwa hiyo simameni, wala msinaswe chini ya kongwa la utumwa."*** Wakati ambapo unapokea ahadi ya Roho, kuna kuwa na uhuru. **2 Kor.3:17** ***"Basi 'Bwana' ndiye Roho; walakini alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru***."

Lengo ni kuuona uso wake:

Gal.5:5 ***"Basi yeye aliyetufanya kwa ajili ya Neno lilo hilo ni Mungu, aliyetupa arabuni ya Roho."*** Ni kwa njia ya Roho tunangojea. **Zab.17:15** ***"Bali mimi nikutazame uso wako katika haki, niamkapo nishibishwe kwa sura yako."***

Kuzishinda tama za mwili:
Gal.5:16-21 yatwambia tukienenda katika Roho hatutazitimiza tamaa za mwili kamwe. Roho Mtakatifu anapoifanya hii kazi ya utakaso katika maisha yetu, hatutatamani tena kuzitimiza tamaa za mwili. Badala yake Roho ataleta tunda katika maisha yetu.
Gal.5:22-23 ***"Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha na amani, upole kiasi, uvumilivu, utu wema, fadhili na uaminifu; juu ya mambo hayo hakuna sheria."*** **Gal 5:25** ***"Tukiishi kwa Roho, natuenende kwa Roho pia."*** Sababu ya kuenenda katika Roho ni kuusulubisha mwili na kisha tunaweza kuufurahia uhuru wa Roho Mtakatifu.

5. Roho Mtakatifu anaweka kipawa chake mwenyewe ndani ya kila mmoja akiwa Mwalimu wetu.

1 Yoh.2:20 ***"Nanyi mmepakwa mafuta ya Yeye aliye Mtakatifu, nanyi mnajua yote."***
a. 27 ***"Nanyi, mafuta yale mliyoyapata kwake yanakaa ndani yenu, wala hamna haja ya mtu kuwafundisha; lakini kama mafuta yake yanawafundisha habari ya mambo yote, tena ni kweli wala si uongo, na kama yalivyowafundisha, kaeni ndani yake."***

Isa.30:20-21 ***"…Lakini Mwalimu wako hatawaficha tena, ila macho yako yatawaona waalimu wako, na masikio yako yatasikia neno nyuma yako, likisema: njia ni hii, ifuateni mgeukapo kwenda mkono wa kulia, na mgeukapo kwenda mkono wa kushoto.'"***

6. Roho Mtakatifu anatupatia nguvu za kuwa mashahidi:

Matendo 1:8 ***"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, nayi mtakuwa mashahidi wangu."***
Matendo 4:31 ***"hata walipokwisha kumuomba Mungu, mahali pale walipokusanyika, pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu wakanena Neno la Mungu kwa ujasiri."***
[Mika 3:8a ***"Bali mimi hakika nimejaa nguvu kwa Roho ya Bwana"*****]**

7. Kuenenda kulingana na Roho:-

Roho wa uzima ndani ya Kristo Yesu
Rum.8:1-4 tunaambiwa tusienende katika mwili bali kulingana na Roho. Kwa maana ***"Roho wa uzima katika Kristo Yesu ameniweka huru kutoka kwa sheria ya dhambi na mauti."***

Kuiweka nia yetu kwa mambo ya Roho:
Rum.8:5 ***"Kwa maana wale waufuatao mwili, huyafikiria mambo ya mwili, bali wale wafuatao Roho huyafikiria mambo ya Roho."***

Ni Roho akaaye ndani yetu atufanyaye kuwa mali ya Kristo:
Rum.8:9-11 ***"Bali ninyi hamko katika mwili bali katika Roho, ikiwa hakika Roho wa Mungu akaa ndani yenu. Na ikiwa awaye yote hana Roho wa Kristo, yeye huyo si wake.***

Roho akaaye ndani ni uzima:
Na Kristo akiwa ndani yenu, mwili umekufa kwa ajili ya dhambi, lakini Roho yenu I hai kwa sababu ya haki.

Anaihuisha miili yetu:
Lakini ikiwa Roho yake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua yesu Kristo kutoka katika wafu ataihuisha na miili yenu, iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu." Nguvu za utakaso wa Roho unaadhiri miili yetu iliyo katika hali ya kufa.

Kwa hiyo tuishi kulingana na Roho:
Rum.8:12-13 ***"Basi, kama ni hivyo, ndugu, tu wadeni, si wa mwili tuishi kwa kufuata mambo ya mwili, kwa maana kama tunanaishi tukifuata mambo ya mwili, mwataka kufa, bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi."*** Tukienenda kulingana na Roho tutaishi. **Aya ya 14** inatwambia kuwa wanaoongozwa kwa Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu. Ni Roho aliyeko ndani yetu anayetushuhudia kuwa sisi ni watoto wa Mungu, **a15-16**.

8. Roho Mtakatifu anatusaidia katika safari yetu kwa kufanya maombi ya kuugua ndani yetu

Rum. 8:26 ***"Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba kama utupasavyo, lakini Roho Mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa."***

AGANO JIPYA:

Gal.3:14 inazungumzia Baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa ***"tupate kupokea Ahadi ya Roho kwa njia ya imani."*** Baraka ya Ibrahimu ni ahadi ya Roho Mtakatifu, kwa Wayahudi na kwa Mataifa pia. Jinsi Petro alivyohubiri Siku ya Pentekoste kwa umati wa Wayahudi, njia ya pekee ya kuja katika Agano Jipya, kuipokea ahadi ya Roho Mtakatifu, ni kwa njia ya Toba, imani katika Kristo Yesu na ubatizo.

Roho Mtakatifu aliahidiwa na Mungu katika manabii:

Ezek.36:26 ***"Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama."*** **Aya ya 25** inazungumzia juu ya kunyunyiziwa maji safi. Hili ni Neno. Tunastahili kupokea moyo mpya na roho mpya. Hii inazungumzia juu ya kuzaliwa ya pili. Mungu katika Agano Jipya ametuahidi kuweka Roho wake ndani yetu, **a27** ***"nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda."*** Katika sheria ya Musa, watu waliamurishwa na sheria. Katika Agano Jipya tunapokea ahadi ya Roho Mtakatifu anayetuwezesha kuitimiza sheria. Ufunguo wa Agano Jipya ni kwamba Mungu ameweka Roho wake Ndani yetu na Roho wake anatuwezesha kutembea kuzishika amri zake na hukumu zake. Tunawezeshwa kuikamilisha safari hii ya kutoka msalabani hadi utukufuni kwa sababu Roho yuko ndani yetu.

Ebr.8:8-13 [nukuliwa katika **Yer.31:31-34**] inazungumzia jinsi Mungu ataiandika sheria yake katika akili zetu na katika mioyo yetu. Mungu anakamilisha haya kwa kumuweka Roho wake ndani yetu. Hakuna Agano Jipya bila damu, lakini ni Roho ndiye anayetuwezesha kuendelea na safari katika Agano Jipya.

Roho Mtakatifu ni ahadi ya Baba (**Matendo 1:4**). Yesu alikuja kufilia dhambi zetu, kuimwaga damu yake kwa kutuosha, ili tuweze kumpokea Roho Mtakatifu.

TAMATI

Ni mungu ndiye atutakasaye kabisa:

1 Thess.5:23 ***"Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo."*** Pale msalabani tunaangamiza matendo ya mwili. Tunakutana na Yesu na tunaokolewa. Nafsi inaanza kufanywa takatifu, inatakaswa, inajazwa na Roho Mtakatifu, kuiwezesha nafsi kuishi na kutembea katika Roho. Roho ya mwanadamu inazaliwa ya pili katika utukufu wa

Mungu kwa sababu Mungu ni Roho na tunamuabudu katika Roho na Kweli, (**Yoh.4:24**). Mwisho wa safari yetu ni utukufuni pamoja na Baba. Safari basi inakuwa safari ya utakaso. Roho Mtakatifu alituleta kwake Yesu, akamfunua Kristo, akaweka upako wake juu yetu tukawa mali yake Kristo, tunaelekea utukufuni.

Utakaso unatuelekeza katika utimilifu katika utukufu:

Juda 1 ***"…kwa hao walioitwa, waliopendwa katika Mungu Baba, na kuhifadhiwa kwa ajili ya Yesu Kristo."*** Mungu Baba anakusudi la kututakasa**.** Mungu baba anaiangalia kwa makini hii kazi yote ya utakaso. Anafanya hivyo kwa damu ya Mwana Wake Yesu, kwa Neno lake na Roho Mtakatifu. Anataka tuwe watakatifu, wakamilifu na bila mawaa mbele zake. **Juda 24-25** ***"Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu. Yeye aliye Mungu pekee, Mwokozi wetu kwa Yesu Kristo Bwana wetu; utukufu una yeye, na ukuu, na uwezo, na nguvu, tangu milele, na sasa, na hata milele. Amina."*** Lengo ni kuingia utukufuni. Tunawezeshawa kufanya hivyo kwa sababu nguvu za Mungu zinatuhifadhi kwa njia ya Roho Mtakatifu; anataka kutusimamisha mbele ya utukufu bila mawaa.

Tukimtazama BWANA katika Roho wa ibada tunabadilishwa katika mfano uo huo:

2 Kor.3:18 ***"Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kiio, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho."*** **Tunabadilishwa**. **Tunageuzwa**.
Tunabadilishwa sura na Roho Mtakatifu.Roho hatutakasi tu, anatuleta pia kutoka kwa kiwango kimoja cha utukufu hadi mwingine hata anavyofanya kazi ndani yetu.

SURA YA 6

KUINGIA KATIKA UTUKUFU

Tumeokolewa kwa utukufu

2 Thess 2:13b-14 ***"Kwa kuwa Mungu amewachagua tangu mwanzo mpate wokovu katika kutakaswa na Roho, na kuiamini kweli, aliyewaitia ninyi kwa Injili yetu, ili kuupata utukufu wa Bwana wetu Yesu Kristo."***

Tumeokolewaje? Katika **kutakaswa na Roho, na kuiamini kweli**.

Kwa nini Mungu alituchagua? Kwa nini alituokoa? Kituo cha haya ambayo tumeitiwa ni nini? **Ili kuupata utukufu wa Bwana wetu Yesu Kristo!** Mungu anataka tuutafute utukufu Wake. Katika maandiko Matakatifu, Mungu anasema hawezi kuushiriki utukufu wake na mwingine. Hii inamaanisha hatenda kushiriki utukufu wake na shetani, au mapepo wachafu, au kiongozi wa dini yeyote, haijalishi watakuwa wamebobea jinsi gani. **Lakini watu Wake watafunikwa na utukufu wa BWANA**, (**Isa.60:1-2**). Mwili wa Kristo unaenda kupokea utukufu wote wa Bwana Yesu Kristo.

KUHATIMISHWA KWA AJILI YA UTUKUFU

Mungu tangu mwanzo aliwachagua mpate wokovu, Aliwachagua pia ili muupate utukufu.

Alituchagua ili tuvikwe na upako wake, ambao hauna kipimo (**Yoh.3:34**)**.** Neno ni kweli (**Yoh.17:17**); tunaokolewa kwa kuiamini ile kweli. Ni Neno na Roho ndiyo hutuongoza hata kuufikia utukufu. Mwisho wa safari ni ***utukufu wa Mungu***. Safari ni kutoka msalabani hadi utukufuni; ili tutakaswe kabisa; na kufanywa kuwa watakatifu kama Yeye alivyo Mtakatifu, (**1Pet.1:16**). Ni safari ya kujitenga kutokana na cho chote kilicho kichafu na kilicho najisi, (**Lawi.11:44-47**)

HENOKO ALIENDA PAMOJA NA MUNGU

Biblia inasema katika **Mwa. 5:24**, kuwa ***"Henoko akaenda pamoja na Mungu, naye akatoweka, maana Mungu alimtwaa."*** **Ebr. 11:5** yasema Henoko alikuwa mtu wa imani na kwamba Mungu alimhamisha moja kwa moja hadi mbinguni asione mauti. Ameshuhudiwa kwamba alimpendeza Mungu. **Ebr.11:6** ***"Lakini pasipo imani haiwezekani, kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini Kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao."***

1) **<u>Henoko alikuwa mtu wa imani</u>.**
   Kwa imani aliushinda ulimwengu, (**1Yoh.5:4**). Kwa imani aliishinda dhambi kwa sababu Biblia inasema hakuona mauti. Mshahara wa dhambi ni mauti, (**Rum.6:23**). Henoko alitwaliwa bila kuona mauti.

2) **<u>Henoko aliingia mbinguni bila kuona mauti</u>.**
   Hii ilikuwa ni fursa ya kipekee kabla ya msalaba. Aliingia utukufuni.

USHUHUDA WAKE HENOKO, MFANO WA KANISA LA SIKU ZA MWISHO.

Henoko ameshuhudiwa katika Maandiko Matakatifu na ushuhuda wa aina hii ni mfano kwa Kanisa la nyakati za mwisho. Kile tunajifunza kutoka kwake Henoko kitatusaidia kujifunza kujua sisi ni nani katika nyakati za mwisho, na ni Kanisa al namna gani BWANA anatazamia katika mwisho w dahari.

Maana ya Jina:

Jina Henoko katika Kiebrania linamaanisha:- SC #2585: ***aliyewekwa wakfu*** *[aliyetawazwa],aliyetolewa, aliyepeanwa; linatoka kwa Neno lingine linalomaaniisha* ***kuwa na nidhamu*** [SC #2596].

Henoko alijitolea kwa ufalme wa Mungu; aliutafuta kwanza ufalme wa Mungu na Haki Yake, (**Matt.6:33**). Aliishi kwa imani; hakujisumbua kwa lo lote, bali katika kila Neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru haja zake zilijulikana na Mungu na amani ya Mungu ilihifadhi nafsi yake na moyo wake katika Yesu Kristo, (**Filipi.4:6-7**). Aliyaweka mawazo yake kwa mabo yaliyo juu, (**Kol.3:1-3**). Alikuwa mwanafunzi wa Neno la Mungu.

Henoko alipewa jina la kinabii kama mmoja aliyetolewa wakfu kwa Mungu. Bwana anataka watu Wake, **Kanisa lake la siku za mwisho, lijitolee na kujiweka wakfu Kwake.** Kila mshiriki wa Kanisa la nyakati za mwisho afanye hatua ya kwanza katika imani yake ya Kikristo katika ubatizo na kujiweka wakfu kwake BWANA.

KUJITOLEA KWA UOVU

Henoko wa kwanza katika Maandiko: uzao usiokuwa wa Mungu

Katika **Mwa. 4** tunampata Kaini mwana wa Adamu alikuwa na mtoto kwa jina Henoko. **a.16** Kaini akatoka mbele za uso wa BWANA. Alitoka mbele ya uso wa BWANA kwa sababu alikuwa mwenye dhambi aliye kataa kutubu. Sio rahisi kusailia katika uwepo wa BWANA ukiwa na dhambi katika maisha yako. Kuna hukumu juu ya dhambi katika nyumba ya Mungu. (mfano. **Matendo 5:1-11**)

Mwa. 4:17 Mzaliwa wa kwanza wa kiume wa Kaini aliitwa Henoko. Huyu Henoko alitolewa wakfu kwa dhambi. Kaini pia aliujenga mji aliouita Henoko. Huu ulikuwa ni mji mzima uliotolewa kwa uovu. Huu ni ***mji wa mtu ambao ni kinyume na Mji wa Mungu***.

Kizazi cha 7 kutoka kwa Adamu katika uzao wa Kaini ni mtu aitwaye Lameki. [Tambua kuwa Henoko katika uzao wa Mungu katika Sethi pia ni wa 7 kutoka kwa Adamu.] Alikuwa amejitwalia wake wawili (**a.19**); akajivuna kuwa alimuuwa mtu na kuwa **atajilipizia kisasi mara sabini na saba**. Huyu ni mtu anayeishi katika mji uliotolewa wakfu kwa ajili ya uovu, ambaye amejitolea kwa uovu kabisa. **Alihalalisha ndoa za wake wengi**; alikuwa na uchungu na kisasi, [kumbuka Yesu alitufunza kusamehe sabini mara saba.]

HENOKO WA PILI: UZAO WA MUNGU

Katika **Mwanzo 5** tunasoma juu ya kizazi cha Sethi.

a.18-19 ***"Yaredi akaishi miaka mia na sitini na miwili, akamzaa Henoko. Yaredi akaishi baada ya kumzaa Henoko mika mia nane, akazaa wana, waume kwa wake."*** Tunajifunza pia kuwa, baba yake Henoko alikuwa mtu wa pili kuishi miaka mingi baada ya Methusela. Pia kuwa **Henoko alikuwa na ndugu na dada**.

a.21 ***"Henoko akaishi miaka sitini na mitano, akamzaa Methusela."*** Methusela ni mtu aliyeishi miaka mingi zaidi katika Biblia. Aliishi miaka 969. ***Henoko alikuwa nabii*** na alimuita mtoto jina la kinabii. ***'Methusela'*** lamaanisha: ***'wakati nitakapo kufa, itatendeka'***. Huyu mtu Methusela alitembea duniani kwa miaka 969, akihubiri ***'wakati nitakapo kufa, itatendeka'***. Hii ilikuwa ni onyo kwa kila mtu kuwa kuna kitu ambacho kinaenda kutendeka kwa kila mtu. Mwaka ambao Methusela alikufa, gharika ikaja. Kwa miaka 969, mwana wa Henoko alikuwa onyo la kinabii kwa wakaaji wa dunia kuwa hukumu inakuja.

a.22 ***"baada ya kumzaa Methusela, Henoko akaenda miaka mia tatu na akazaa wana, waume kwa wake."*** Huyu Henoko alikuwa **ametolewa wakfu katika uzao wa Mungu**. **Ametolewa kwa ajili ya BWANA**. Biblia inaandika kuwa kwa miaka 300 ***'alienda na Mungu'.*** **Henoko alikuwa mtu wa jamii**, alikuwa na wana na binti. Hili halikuweza kumzuia ketembea na Mungu. **a.23-24** ***"Siku zote za Henoko ni miaka mia tatu na sitini na mitano. Henoko akenda pamoja na Mungu, naye akatoweka, maana Mungu alimtwaa."*** Kuelewa haya zaidi tutahitaji kuangalia katika Waraka kwa **Waebrania 11:5** ***"Kwa imani Henoko alihamishwa, asije akaona mauti, wala hakuonekana, kwa sababu Mungu alimuhamisha; maana kabla ya kuhamishwa alikuwa ameshuhudiwa kuwa ameshuhudiwa, kwamba amempendeza Mungu."***

Henoko hakuona kifo! Mungu alimtwaa! Baada ya kuenda na Mungu miaka 365, alitwaliwa; alibadilishwa sura, [twaliwa]. Kwa nini Henoko alitwaliwa? Kwa maana alishuhudiwa ***'kuwa amempendeza Mungu'.*** Alienda na Mungu kwa karibu sana kuwa ***mgawanyiko kati ya mbingu na dunia haukuwepo tena.***

KATIKA KRISTO MBINGU NA NCHI HUJUMLISHWA

Katika **Efe.1:10** mojawapo ya Baraka za mbinguni ambayo tumepokea kutoka kwake Kristo ni ***"kuleta madaraka ya wakati mtimilifu atavijumlisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia. Naam, katika Yeye huyo."*** Henoko anatupatia yale yaliyotendeka katika aya hii. Henoko alitwaliwa. Haya yalitendekaje? Pazia kati ya mbingu na dunia ilifunguka kwa hivyo hakuna mgawanyiko tena kati ya Henoko kuenda hapa duniani na kuenda mbinguni.

Ni vitu gani vitakavyo jumlishwa katika Efe.1:10? Vitu vyote vilivyomo katika Kristo.
Ni vitu gani vilivyomo katika Kristo duniani katika mwisho wa nyakati? Kanisa. Wakati Kanisa linapobadilishwa, kutakuwa na dhihirisho la kujumlisha vitu vyote katika Kristo vilivyomo mbinguni na duniani, (**1 Thess.4:16-17**).

BIBLIA INATWAMBIA NINI KUHUSU KANISA LA NYAKATI ZA MWISHO?

1 Kor.15:51-52 ***"Angalieni, nawaambia ninyi siri hatutalala sote, lakini wote tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu , nasi tutabadilika,"*** Tazama pia **1 Yoh.3:2-3**.

1 Thess. 4:14-17 ***"Maana ikiwa tunaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na wale walio lala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye.*** [Wale ambao wameenda kuwa na Bwana – *'waliolala katika Kristo* – watarudi pamoja naye katika miili yao ya roho] ***Kwa maana twawaambieni haya kwa Neno la Bwana, kwamba sisi tuliohai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana Mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; na waliokufa katika Kristo, watafufuliwa kwanza.***

Kisha sisi tuliosalia tutatwaliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. [hii inazungumzia juu ya miili ya wale waliotutangulia na ambao wanarudi na Bwana katika **a**.**14.**]

> **Kutwaliwa – *harpadzo* (har-pad-zoe)** Strong's #726; *kunyakua, kutwaa, kuchukuwa kwa nguvu.* Neno linaelezea juu ya tendo la Roho Mtakatifu katika kumchukua Filipo kutoka sehemu moja hadi nyingine (**Matendo 8:39**) na Paulo kuchukuliwa hadi Paradiso (**2 Kor.12:2-4**). Linazungumzia hali ya kutumia nguvu fulani kukichukuwa kitu.

Kunakuja wakati ambapo Wakristo wanaoishi duniani, ambao wanaoenda na Mungu, jinsi ambavyo Henoko alivyoenda na Mungu, watatwaliwa na kumlaki Bwana mawinguni. Vitu vyote katika Kristo vitajumlishwa kuwa naye milele.

NI VYETI GANI AMBAVYO HENOKO ALIKUWA NAVYO VILIVYOMWEZESHA KUTWALIWA NA MUNGU?
Alienda na Mungu kwa miaka 300. Ushuhuda wa Henoko ni aina ya Kanisa la nyakati za mwisho. **Aliwezeshwa kutakaswa kabisa. 1Thess.5:23 *"Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa, nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo."***

NI KWA MSINGI GANI TUTATWALIWA KUMLAKI BWANA MAWINGUNI?
Kwa sababu tunaenda na Mungu. Yesu alituonya kwamba tusipokuwa tayari kwa kurudi Kwake ***tutaikosa***. Yesu alituonya kwamba atakuja kama mwivi usiku na hatuijui saa ile mwizi atatushambulia, (**2 Pet.3:10, Math.24:43**).

Katika mfano wa wanawali 10, kanisa lote lili lala lakini sauti ikasikika ***'Tazameni Bwana Arusi yuaja'***, (**Math.25:1-13**), na kanisa likaamka usingizini, bali ni watano tu walikuwa wako tayari na hawakuhitaji maandalizi zaidi. Walikuwa tayari kuufwata mwito. Lakini wale watano wengine waliondoka kwenda kuazima mafuta na waliporudi mlango ulikuwa tayari umefungwa.

Bwana anatuhimiza sisi Kanisa lake tuwe tayari kwa kurudi kwake. Anataka Kanisa Lake litoke Usingizini. Mambo hayako tena jinsi yalivyokuwa. Matukio duniani yameruhusiwa kutendeka kama ishara ya kuliamsha Kanisa. Mungu Mwenyezi yuko anakamilisha mpango wake wa ajabu katika maisha yetu.

MUNGU ANALIANDAA KANISA LAKE

Kanisa lake haliwezi kukamilika, [kanisa tukufu ambalo anarudia] mpaka kuwe na Myahudi na Myunani katika mwili mmoja.
Efe.2:14 *"Kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kile kiambaza cha kati kilichotutenga."* Yesu alikibomoa kile kiambaza cha kati kilichotenganishaMyahudi na Myunani na kumfanya mtu mmoja mpya, (**a.15-16**). Kuna mwili mmoja tu wa Kristo! Tarajia kuharakishwa kwa wokovu kwa Wayahudi – Wayahudi wengi wataokoka – mabaki waliosalia kuwa waaminifu kwa Mungu kwa miaka 2000**.**

SIRI NI NINI?

Katika **Efe. 3** Paulo anafundisha juu ya siri iliyohubiriwa katika vizazi vya zamani ambayo sasa imefunuliwa kwa njia ya kuhubiriwa Injili. Siri ni kwamba **Kanisa linajumlisha Myahudi na Myunani**. **Kuna mwili mmoja tu wa Kristo**. Ni huo Mwili, utajulisha falme na mamlaka

katika ulimwengu wa Roho kupitia kwa hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi, (**Efe.3:9-10)**. Huu ndio Mwili, unaojumlisha Myahudi na Myunani pamoja ambalo Krisyto analirudia. Yeye harudi kulichukuwa kanisa la Wayunani pekee yao kulipeleka mahali Fulani kwa kipindi Fulani, na kisha kuliinua kanisa la Wayahudi litakalo hubiri Injili katika kipindi hicho. Tafsir kama hiyo kwa neon la Mungu, yaonyesha ukosefu wa ufahamu wa siri ya kanisa ambalo linafundishwa katika **Efe 2** and **3**.

Katika **Efe 5** inabaishwa wazi kwamba Yesu Kristo anajiandalia Kanisa tukufu lisilo na ila wala kunyanzi.

MABADILIKO YA MILENIA

Mungu anataka tufahamu matendo yasiyo kuwa ya kawaida ambayo yanatendeka sasa. Kanisa la nyakati za mwisho litaamka na kumlaki Bwana mawinguni, ni kanisa linalotembea karibu sana na Mungu, jinsi Henoko alivyo kuwa. Henoko *'hakuona mauti kwa sababu Mungu alimtwaa*. Tukio hili lilitendeka mwiso mwisho wa Milenia ya kwanza.

<u>Mungu hufanya kazi katika Milenia.</u>

Mungu **alimuumba Adamu wa Kwanza** karibu miaka elfu sita iliyopita. Katika mwisho wa millennia ya Kwanza kutoka kuumbwa kwa Adamu, ***Henoko*** **alihamishwa** [**miaka 987** kulingana na **Mwan.5**].

Miaka 2000 kutoka kwa Adamu, ***Ibrahamu*** **aliitwa** kutoka [Ur ya Wakalidayo] na kuitwa katika kusudi la Mungu la milele. Kutoka kwa Ibrahimu atakuja Mbegu ya ahadi ***"kuponda kichwa cha nyoka"***. Kupitia kwake Ibrahimu, Mungu alifanya jambo jipya duniani!

Miaka 3000 kutoka kwa Adamu, ***Mfalme Daudi*** **anatwala taifa la Israrei**. Kulikuwa na dhihirisho la ufalme wa Mungu duniani katika maisha na utawala wa Daudi – mfano wa Kristo na Ufalme Wake!

Miaka 4000 kutoka kwa Adamu, ***Kristo anazaliwa***. Kwa kufa na kufufuka tena kizazi kipya kinaanzishwa ambacho kitakamilishwa wakati atakaporudi tena kuunganishwa na kanisa lake tukufu. Kizazi hiki ni cha siku mbili za mileni – siku moja kwa Bwana ni kama miaka elfu (**2Pet.3:8**). Yesu akasema, ***"nendeni mkamwambie Yule Mbweha, Tazama Leo na kesho ninatoa pepo na kuponya wagonjwa, siku ya tatu nakamilika."*** (**Lu.13:32**). Mika elfu mbili ya kizazi hiki karibu kukamilika.

Mabadiliko ya Milenia, ambayo yanakamilishwa kwa matukio kama Kuzaliwa kwa Masihi, Mwito wa Ibrahimu, Kanisa kubadilishwa, ni **jambo la mabadiliko ya kizazi.** Milennia inachukuwa kizazi katika ukamilifu wake. Sisi ni kizazi kile kitakacho shuhudia kurudi kwake Bwana. Ishara za kurudi kwake siku za mwisho zinatimilika katika kizazi chetu. Je, ukotayari kwa kurudi kwake? Je, unaendelea ***"kujitakasa"***? (**1Yoh.3:3:2-3**)

KUJIANDAA KWA AJILI YA KURUDI KWAKE

Henoko ni Yule aliyewekwa wakfu, nabii wa Mungu aliyejitolea na kwa miaka 300 aihubiri haki; alienda na Bwana. Halafu akatwaliwa. Wakati unakuja ambapo tutaipokea sauti ya parapanda ya Mungu na sauti ye malaika mkuu, na tutatwaliwa (**1 Thess.4:16-17**). Sauti ya paragumu inalia sasa ***"inua vichwa vyenu, wokovu wenu umekaribia."***

Katika **Luka 21:28** Yesu anatuonya ***"wakati mambo haya yanapoanza kutendeka, inua vichwa vyenu, maana ukombozi wenu umekaribia."*** Wakati tunashuhudia mikasa

inayotendeka karibu nasi, tunastahili kuinua macho yetu na kusema, *'asante Yesu ya kuwa unarudi hivi karibuni na Bwana nataka niwe tayari!'* Tunastahili kuwa kama Henoko ***'tukienda na Mungu***, tukiwa na imani kama ya Henoko na kushuhudiwa kama Henoko ***'kuwa tunampendeza Mungu'*** katika yote tufanyayo.
Kol.3:17 ***"Na kila mfanyalo kwa tendo au maneno, fanyeni yote kwa jina lake Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye."***

Bibli iko wazi kunena kuwa kuna kizazi ambacho hakitaonja kifo. Roho Mtakatifu analiandaa Kanisa lisilo na ila wala kunyanzi. Henoko alikuwa mbegu ya unabii ya kanisa la siku za mwisho ambalo litatwaliwa bila kuonja mauti. Hili litatendeka kwa sababu kanisa hili lilikuwa likienda na Mungu na hakuna kile kiambaza cha kati kilichotutenga kati ya mbingu na nchi.

TUKO TUNATUKUZWA

Ebr.6:4-5 inaelezea mambo fulani ambayo Mungu anatueleza katika Neno lake ambayo tayari tunayashriki, ambayo yanatuandaa kukaa katika utukufu Naye. Mwandishi anasema, ***"Tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu."*** Tukaze mwendo ili tuufikilie utukufu! Tunaelekea katika utimilifu:- tukiwa: ***tumetiwa nuru***, yaani, kuzaliwa ya pili (**Yoh.3:6**)

> ***kuonja kipawa cha mbinguni***, Yesu ni mate ulioshuka kutoka juu (**Yoh.8:41**)
> ***kuwa washirika wa Roho Mtakatifu;*** tumebatizwa kwa Roho Mtakatifu (**Matendo 1:5**)
> tumeonja neno zuri la Mungu***;*** Neno lake li hai na lina nguvu (**Ebr.4:12**)
> ***tumeonja uweza wa kizazi kinachokuja;*** tunashuhudia kwamba tumeshuhudia uweza Wake Mkuu.

Hakuna kurudi nyuma tena katika safari yetu. Usiondoe mkono wako kwenye jembe (**Lu.9:62**). Usigeuke nyuma kama mke wa Lutu. ***"Tukaendelee kumjua Bwana,"*** **Hosea 6:3**. ***"Baada ya siku mbili atatufufua; siku ya tatu atatuinua, nasi tutaishi mbele zake,"*** **Hos.6:2**.

LAKINI MMEPOKEA UPAKO

Henoko alikuwa mtu aliyepakwa; alijua jinsa ya kukaa ndani ya Yesu na jinsi ya kukaa na upako. **1 Yoh.2:20** ***"Nanyi mmepakwa mafuta ya yeye aliye Mtakatifu nanyi mnajua yote."***
1 Yoh.2:27 ***"Nanyi, mafuta yale mliyoyapata kwake yanakaa ndani yenu, wala hamna haja ya mtu kuwafundisha, lakini kama mafuta yake yanavyowafundisha habari za mambo yote, tena ni kweli wala si uongo, na kama yalivyowafundisha, kaeni ndani yake."***

Kanisa la siku za mwisho linatakiwa liwe kanisa lenye kujaa Upako. **Math. 25:1-13** anatwambia juu ya mfano wa wanawali kumi. Bikira ni Yule ambaye ameposwa na Kristo. Hawa wanawali wanawakilisha nusu ya kanisa la Kristo lilikuwa tayari kumpokea Bwana arusi aliporudi. Tunastahili kuwa tayari, tuwe vyombo vilivyojaa mafuta maana hatuijui siku wala saa ya kuja kwake. Kama Henoko tunatakiwa tutembee katika hayo mafuta sisi wenyewe.

HENOKO ALIKUWA WA SABA KUTOKA KWA ADAMU, ALITABIRIWA

Mwisho wa kutajwa kwake Henoko katika Maandiko Matakatifu ni katika **Yuda 14**. Hapa tunajifunza zaidi kuhusu ushuhuda wake ambao ni funzo kwa kanisa la siku za mwisho.
v.14-15 ***"Na Henoko mtu wa saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya unabii juu ya hao, akisema, Angalieni, Bwana alikuja na watakatifu wake, melfu maelfu, ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuwaadhibisha wote wasiomcha Mungu, kwa ajili ya kazi zao za upotevu walizozitenda bila kumcha Mungu, na kwa ajili ya maneno magumu yote ambayo hao wenye dhambi wasiomcha Mungu wameyanena juu yake.'"***

1. Henoko ni kizazi cha saba baada ya Adamu. Saba ni nambari ya ***utimilifu*** katika Maandiko Matakatifu. ***Henoko ni mfano wa mtu mkamilifu***, (**Efe.4:13**). Yeye ni mfano wa Kristo, bali pia ni mfano wa kanisa kamilifu siku za mwisho. Yesu aliandikia makanisa saba katika **Ufu.2-3**. Yohana alimuona Yesu katikati ya makanisa saba katika **Ufu.1:13**. Kanisa linapofikilia utimilifu, Kristo atafunuliwa wazi hapa duniani kupitia kwa kanisa na atakapoinuliwa atawavuta watu wote Kwake Mwenyewe. (**Yoh.12:32**).

2 ***'Alitabiri'***. Kanisa la siku za mwisho ni la unabii ambalo litatabiri Neno la Mungu kwa Mataifa. Watu wa Kanisa la siku za mwisho watanena kiunabii na kuutangazia ulimwengu kuwa kurudi kwake Bwana ni karibu. **Math.24:14** ***"Tena habari njema ya Ufalme, itahubiriwa katika ulimwengu wote kama ushuhuda kwa mataifa yote, hapo ndipo ule mwisho utakapokuja."***

HAWA WATU HENOKO ANAZUNGUMZIA NI KINA NANI?

Juda 4 ***"Kwa maana kuna watu waliojiingiza kisiri, watu walioandikiwa tangu zamani hukumu hii, wabadilio neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi, hao humkana yeye aliye pekee yake Mola, na Bwana wetu Yesu Kristo."***
Hawa ni wale wanaomkana Yesu Kristo.

Katika **Math.24:5** Yesu anatuonya, akinena habari ya siku za mwisho, ***"Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, mimi ni Kristo na watawadanganya wengi."***
Hawa ni waalimu wanaosema, *'Yesu ni Kristo'* lakini wanawadanganya wengi katika mafundisho yao. Dhambi ya kanisa la siku za mwisho ni kwamba kutakuwa na wale watakaokataa kuamini. Hawatakuwa wakihubiri kweli. Kuna wale wanaotembea katika kutokuamini, kama jinsi tu wale wapelelezi kumi walivyohubiri kutokuamini kwa wana wa Israeli baada ya kuipeleleza Nchi ya Ahadi. Waliiona Nchi ya Ahadi lakini wakaitafsiri kimwili. Wakaliongoza taifa zima katika dhambi ya kutokuamini. Matokeo yakawa ni kifo kwa kizazi chote.

Kuna wale waliomo Kanisani leo ambao hupuuza mafunzo ya Biblia, wakikana ukweli wa kitabu cha Mwanzo, wakiwakubalia mabasha/shoga na washerati katika kanisa na hata kuwatawaza kuwa wahudumu wake.

KUNA MKUTANO NA MUNGU

Mungu analiandaa kanisa lake la siku za mwisho kwenye mkutano wa ajabu. Mungu wakati wote amekuwa na mahali pa kukutana na watu Wake. Mungu alishuka katika Mlima Mtakatifu na akakutana na watu Wake. Sikukuu za waisraeli zilikuwa za wakati wa watu kukusanyika mahali pa mkutano. Hizi sikukuu zimetimizwa katika Kristo. Mungu tayari amekutana nasi katika Sikukuu ya Pasaka – tumeokolewa kwa njia ya kufa na kufufuka kwake Yesu. Roho Mtakatifu alikuja kutujaza na hivyo kuitimiza Pentekoste. BWANA anaenda kuujaza ulimwengu na utukufu wake kwa njia ya Kanisa la siku za mwisho lenye utukufu na kisha tutainuka na kukutana na BWANA mawinguni.

Maombi ya watu Wake yatamsababisha Mungu kushuka ili akutane na watu Wake tena. Mpango wake Mungu juu ya watu wake utatimizwa kikamilifu. Hizi ni siku za utimilifu. Tunaishi ukingoni mwa nyakati na kama Henoko tunatakiwa kuenda na Mungu kama alivyofanya ili tutakaswe kabisa na tuwe tayari kumpokea.

TAMATI

1Thes. 5:23 ***'Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa, nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo."*** Kusudi kuu la Mungu ni tutakaswe kabisa, roho, mwili na nafsi. Mungu anataka tuingie utukufuni kama Henoko. Mungu anataka tuhifadhiwe bila lawama hata kurudi kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Ni wakati wa kujitayarisha! Ni wakati wa kuamka! Ni wakati wa kuvikwa katika utukufu wa Bwana wetu!

Juda 24 ***"Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu."*** Mungu anaenda kufanya hii kazi ndani Yetu. Roho Mtakatifu yupo kazini ndani yako kupenda na kufanya mapenzi ya Baba. Ameahidi kuikamilisha kazi ambayo ameanza: ***"hao alio wahesabia haki, hao pia alitukuza."*****na ameteua huduma kanisani ya kumjenga kila mteule, kwa ajili ya kuuleta mwili wake Kristo katika utimilifu,** *"kuwaonya watu wote na kuwafundisha watu wote katika hekima, ili tupate kumleta kila mtu mkamilifu katika Kristo."* **(Kol.1:28).**

Efe. 5:27 ***"Apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaaa."*** Haja ya Mungu ni Kanisa tukufu, lisilo kuwa na mawaa. Bwana Yesu mwenyewe yuko analiandaa kanisa Lake: ***"Alitakase na kiliosha kwa maji katika Neno."***

Yoh.17:22 ***"Nami utukufu ule ulionipa, nimewapa wao, ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja."*** Yesu alimuomba Baba aweke utukufu ambao ulikuwa wake kwa kanisa Lake.

Isaya 60:1-2 ***"Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, na utukufu wa Bwana umekuzukia! Maana, tazama, giza litaifunika dunia, na giza kuu litazifunika kabila za watu. Bali Bwana atakuzukia wewe, na utukufu wake utaonekana juu yako."***